MADA:

# KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI CHINI YA MFUMO WA 8-4-4:- Utafiti katika jiji la Nairobi

NA:- FLORENCE MUGURE MAINA

"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya 'MASTER OF ARTS' katika chuo kikuu cha Nairobi."

JUNI 1992

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0146787 7

## TABARUKU

Kwa mpenzi mume wangu, E.N. Wamakima, mtoto wangu mpenzi Dianah Wamakima na mamangu Maria N. Karanja.

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijatolewa kwa mahitaji ya digrii katika chuo kikuu kingine chochote

_______________________________

Florence Mugure Maina
(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa chuo kikuu

_______________________________

Prof. Mohammed H. Abudulaziz

_______________________________

Mr. Mungania B.G.

## YALIYOMO


| | | Ukurasa |
|---|---|---|
| Yaliyomo | | (i) |
| Shukrani | | (ii) |
| Muhtasari | | (iii) |

SURA YA KWANZA

| | | |
|---|---|---|
| 1.0 | Utangulizi | 1 |
| 1.1 | Somo la utafiti | 2 |
| 1.2 | Madhumuni ya tasnifu | 3 |
| 1.3 | Sababu za kulichagua somo hili | 4 |
| 1.4 | Upeo wa tasnifu | 5 |
| 1.5 | Yaliyoandikwa kuhusu swala hili | 6 |
| 1.6 | Msingi wa kinadharia | 11 |
| 1.7 | Njia za utafiti | 14 |
| 1.8 | Njia za kuchagua sampuli | 15 |
| 1.9 | Haipothesia | 17 |
| | Tanbihi | 18 |

SURA YA PILI

| | | |
|---|---|---|
| 2.0 | Utangulizi | 19 |
| 2.1 | Sera ya lugha katika elimu-: Kabla ya uhuru | 19 |
| 2.2 | Sera za lugha katika elimu-: Baada ya uhuru | 28 |
| 2.3 | Kiswahili katika mfumo wa 8-4-4 | 33 |

| | | |
|---|---|---|
| 2.4 | Vifaa vya kufundishia na walimu | 36 |
| 2.5 | Hitimisho | 38 |
| | Tanbihi | 39 |


SURA YA TATU


| | | |
|---|---|---|
| 3.0 | Utangulizi | 40 |
| 3.1 | Matokeo ya hojaji | 41 |
| 3.2 | Ugunduzi wa utafiti huu | 42 |
| 3.2.1 | Mgawo wa vipindi vya kiswahili | 42 |
| 3.2.2 | Vifaa vya kufundishia | 43 |
| 3.2.3 | Silabasi | 46 |
| 3.2.4 | Hisia za wanafunzi kuhusu kiswahili | 52 |
| 3.2.4.1 | Umuhimu wa kiswahili kwa wanafunzi | 53 |
| 3.2.4.2 | Usomaji wa magazeti | 56 |
| 3.2.4.3 | Usikizaji wa radio | 58 |
| 3.3 | Uchanganuzi wa Data | 61 |
| 3.4 | Matatizo yanayokabili kiswahili na matatuzi yake | 66 |
| 3.4.1 | Tatizo la vitabu | 66 |
| 3.4.2 | Tatizo la walimu | 67 |
| 3.4.3 | Tatizo la kuunganisha somo la 'Fasihi ya Kiswahili' na 'Lugha ya Kiswahili' | 68 |
| 3.4.4 | Wazazi kufikiria kuwa kiswahili hakifai | 69 |


HITIMISHO


| | | |
|---|---|---|
| 4.0 | Utangulizi | 70 |
| 4.1 | Yaliyobainika kutokana na data | 70 |

## YALIYOMO

| | | |
|---|---|---|
| | | Ukurasa |
| Yaliyomo | | (i) |
| Shukrani | | (ii) |
| Muhtasari | | (iii) |
| **SURA YA KWANZA** | | |
| 1.0 | Utangulizi | 1 |
| 1.1 | Somo la utafiti | 2 |
| 1.2 | Madhumuni ya tasnifu | 3 |
| 1.3 | Sababu za kulichagua somo hili | 4 |
| 1.4 | Upeo wa tasnifu | 5 |
| 1.5 | Yaliyoandikwa kuhusu swala hili | 6 |
| 1.6 | Msingi wa kinadharia | 11 |
| 1.7 | Njia za utafiti | 14 |
| 1.8 | Njia za kuchagua sampuli | 15 |
| 1.9 | Haipothesia | 17 |
| | Tanbihi | 18 |
| **SURA YA PILI** | | |
| 2.0 | Utangulizi | 19 |
| 2.1 | Sera ya lugha katika elimu-: Kabla ya uhuru | 19 |
| 2.2 | Sera za lugha katika elimu-: Baada ya uhuru | 28 |
| 2.3 | Kiswahili katika mfumo wa 8-4-4 | 33 |

4.2 Maoni na mapendekezo 75
4.3 Matatizo ya utafiti 79
MAREJEO 81
KIONGEZO 87

SHUKRANI

Ningependa kuzitoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu, Profesa Mohammed H. Abudulaziz na Bw. Gichobi Mungania, mwongozo na mashauri yao ndiyo msingi na matokeo ya kazi hii.

Shukrani zangu pia ni kwa mwenyekiti wa idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika Bi. Lucia Omondi na wahadhiri wote wa idara hii kwa kunipa moyo wakati wa kuandika kazi hii na katika masomo yangu.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu, tuliodarisi pamoja kwa miaka hiyo miwili, Baru, Swaleh, Wamitila na Young. Usaidizi wenu uliniinua kila nilipoonyesha dalili za kufa moyo. Baru kwa mawaidha na mashauri yake ya kiusomi na ya kirafiki. Yalinitia moyo wa kujibidiisha kila nilipokuwa karibu kuzama katika ushinde. Asante Sana.

Shukrani nyingi kwa mamangu mpenzi Maria N. Karanja kwa maombi yake ya kila siku na usaidizi wake wa kifedha.

Shukrani kwa mtoto wangu mpenzi Dianah kwa uvumilivu wake na maombi yake kila alipoona nimengojeka.

Napenda kumshukuru kwa dhati mume wangu E.N. Wamakima kwa uvumilivu, mapenzi yake na kunipa moyo wakati nilipokuwa masomoni. Ama ulimwengu ungenihukumu kama ningesahau kumshukuru kwa kugharimia masomo yangu ya digrii ya uzamili.

Mwisho, namshukuru Abescondita Khagai kwa kunipigia chapa kazi hii.

## MUHTASARI

Tasnifu hii ni utafiti juu ya Kiswahili katika shule za upili chini ya mfumo wa 8-4-4 uliofanyiwa katika jiji la Nairobi. Madhumuni yake ni kuangalia masiala yanayohusu Kiswahili katika shule za upili chini ya mfumo wa 8-4-4.

Imegawanyika katika sura nne. Katika sura ya kwanza kuna mada ya tasnifu, madhumuni ya tasnifu, sababu za kuchagua somo, upeo wa kazi hii, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu swala hili, njia za utafiti, matatizo ya utafiti, njia za kuchagua sampuli na mwisho haipothesia.

Sura ya pili ni maelezo juu ya sera za lugha ya elimu nchini Kenya kabla na baada ya uhuru, Kiswahili Katika mfumo wa 8-4-4 na vile vile mambo yapaswayo kuzingatiwa katika utekelezaji wa mradi mpya. Katika kazi hii tutatilia maanani somo la Kiswahili.

Sura ya tatu ni matokeo ya utafiti kwa jumla. Ina matokeo ya hojaji na uchanganuzi wa data. Pamoja na matatizo na yanayokikabili Kiswahili na matatuzi yake .

Sura ya nne, ni hitimisho ambayo zaidi ni maoni na mapendekezo ya mtafiti juu ya maswali mbali mbali yanayotokana na data iliyokusanywa katika utafiti.

Marejeo yametolewa baada ya sura ya nne na mwisho kabisa ni nakala ya hojaji iliyotumiwa kama kiongezo.

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Tangu nchi ya Kenya ipate Uhuru mwaka wa 1963 hadi 1985, nchi hii imekuwa ikifuata mfumo mmoja wa elimu, mfumo huo ulikuwa ni 7-6-3. ama 7·4·2·3

Mfumo mpya wa elimu wa 8-4-4 ni zao la kamati iliyoteuliwa ili kuchunguza uwezekano wa kuanzishwa kwa chuo kikuu cha pili hapa nchini. Kamati hii ambayo iliongozwa na Profesa Mackay ilipendekeza mambo kadha wa kadha kuhusu mfumo wa elimu hapa nchini. Mojawapo ya mapendekezo ya kamati hii ni kuanzishwa kwa kitivo cha taaluma ya jamii, utamaduni na maendeleo, ambacho kingefundisha lugha za Kiafrika ikiwepo lugha ya Kiswahili na lugha nyinginezo za Kenya.

Serikali iliyakubali mapendekezo ya kamati hii mnamo mwaka wa 1982. Mojawapo ya mabadiliko makubwa ambayo yanatokana na mfumo huu ni kule kutiliwa mkazo somo la Kiswahili na kufanywa kuwa somo la lazima katika shule za msingi na katika shule za Sekondari vile vile.

Hapo awali kulikuwa na msisitizo mdogo sana wa somo la Kiswahili katika shule. Isitoshe, Kiswahili kilikuwa somo la hiari. Haya yote pamoja na kuwa hakikutahiniwa kulifanya somo hili kupuuzwa na kudunishwa sio tu na baadhi ya walimu, bali hata na wanafunzi. Haya yote yana misingi yake katika historia. Wakati wa ukoloni, 'lugha ya Kiswahili' ilipuuzwa

na hata baada na nchi kujipatia uhuru, serikali ya Kenya haikuonekana kuwa na msimamo thabiti kuhusu lugha. Hivyo kiingereza kiliendelea kupewa umuhimu, huku Kiswahili kikididimizwa. Hata hivyo jambo hili halikufanikiwa kwani Kiswahili hakikubali kuzama bali kiliendelea kuibuka.

Kwa wakati huu, mambo yaonekana yamebadilika. Kama tulivyosema hapo awali, kupitia kuanzishwa kwa mfumo wa elimu wa 8-4-4 Kiswahili kimefanywa somo la lazima na la kutahiniwa katika shule za upili.

Madhumuni ya somo hili kama yalivyoratibiwa kwenye silabasi ya shule za upili yaonyesha dhahiri kwamba hayawezi kufikiwa bila ya kiazi ngumu za kiakademia kutoka kwa walimu na mwanafunzi walio na nia na motisha ya kusoma somo hili.

## 1.1 SOMO LA UTAFITI

Katika tasnifu hii somo letu la utafiti ni Kiswahili katika shule za upili chini ya mfumo wa 8-4-4.

Tunanuia kuangalia masiala yanayohusu Kiswahili katika shule za upili hasa tukitilia maanani sera tofauti za elimu hapa nchini Kenya.

Jiji linalofanyiwa utafiti ni jiji la Nairobi.

Utafiti wetu utajikita katika kuangalia masiala yaliyomuhimu kusingatiwa ili kuimarisha somo la Kiswahili katika shule za upili.

Tutachunguza na matatizo yanayokumba Kiswahili pamoja na matatuzi yake.

Kama tulivyosema katika sehemu ya 1.0 Kiswahili kwa wakati huu ni somo la lazima na la kutahiniwa. Hapo awali somo hili lilikuwa la hiari katika shule za upili. Hivyo ili kuinua hadhi ya lugha hii katika shule kuna mambo muhimu ambayo kwayo yanapaswa kutiliwa maanani.

## 1.2 MADHUMUNI YA TASNIFU

Kiswahili kwa wakati huu kinatiliwa mkazo katika mfumo wa elimu wa 8-4-4. Tofauti na mfumo wa elimu wa hapo awali wakati Kiswahili hakikutahiniwa, sasa somo hili linatahiniwa kama masomo mengine. Kwa mujibu huu tunadhamiria kuchunguza Kiswahili katika shule za upili chini ya mfumo wa elimu wa 8-4-4.

Katika utafiti wetu tunanuia kuchunguza masiala ambayo ni muhimu kuzingatiwa ili kuimarisha somo la Kiswahili katika shule za upili. Kwa mfano, tutachunguza mgawo wa vipindi vya Kiswahili, silabasi iliyotayarishwa kwa minajili ya shule za upili na vifaa vya kufundishia somo hili. Mambo haya kwa kiasi fulani yataathiri Kiswahili katika shule za upili.

Vile vile tunanuia kuchunguza matatizo yanayokabili Kiswahili katika kiwango hiki cha elimu. Jambo hili litatuongoza katika kuchuguza mbinu ambazo zinaweza kutumika ili kukuza Kiswahili zaidi katika shule za upili.

Mwisho, ni dhamira yetu pia kupata maoni na mapendekezo kutoka kwa watu mbali mbali.

## 1.3 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO HILI

Serikali ya Kenya ilipitisha Kiswahili kuwa lugha ya taifa mnamo mwaka wa 1969. Kiswahili vile vile ni lugha sambazi katika sehemu kubwa ya Bara La Afrika. Pia kwa wakati huu, Kiswahili ni somo la lazima katika mfumo wa elimu wa 8-4-4. kwa muda mrefu somo hili lilikuwa la hiari katika mfumo wa elimu wa hapo awali wa 7-6-3.

Tumeona kwamba, ni utafiti mdogo sana umewahi kufanywa kuhusu Kiswahili katika shule za upili. Nyingi ya kazi hizo ni makala yaliyoandikwa miaka mingi, bila shaka kuna mabadiliko mengi sana ambayo yametokea tangu wakati huo.

Sababu nyingine iliyotuelekeza kuchagua somo hili ni kwamba hamna utafiti ambao umefanywa kuhusu Kiswahili katika shule za upili ukinuia kuangalia masiala muhimu yanayopaswa kuzingatiwa chini ya mfumo wa elimu wa 8-4-4..

Tulinuia pia kupata maoni kutoka kwa walimu, wanafunzi na wataalam wa elimu kuhusiana na somo hili tangu lifanywe somo la lazima. Jambo hili litatuelekeza kutambua matatizo yanayozuia uimarikaji wa Kiswahili katika shule za upili.

Tunatumaini kwamba kazi hii itawasaidia walimu na wachunguzi walio nyanjani. Vile vile ni makisio yetu kuwa kazi hii itasaidia serikali na wale waliokabidhiwa jukumu la kufafanua na kupanga sera na upangaji wa lugha hapa nchini Kenya.

## 1.4 UPEO WA TASNIFU

Tasnifu hii inajikita katika kuangalia Kiswahili katika shule za upili chini ya mfumo wa 8-4-4.Utafiti huu utafanywa katika jiji la Nairobi pekee. Hatutaingilia kulinganisha na mji au miji mingine.

Kwanza, wakati uliotengewa kazi hii ni mchache sana. Huenda kazi ya kiulinganishi isikamilike kwa wakati ufaao.

Pili, utafiti huu haukugharamiwa na chuo kikuu ama shirika lo lote kutoka nje. Kazi hii inawajibika kuchunguza masiala yaliyo muhimu ili kuimarisha somo la Kiswahili katika shule za upili. Tutaangalia mambo kama mgawo wa vipindi, vifaa vya kufundishia na mengineyo.

Kazi hii haitaingilia kwa undani swala la ufundishaji wa Kiswahili; kwa mfano, si jukumu la kazi hii kuchunguza jinsi ufundishaji unavyoendeshwa darasani. Ili kupata matokeo ya kazi kama hii itatulazimu tuchukue muda mrefu zaidi.

Tunatumaini kwamba mambo yote na kauli zote zitakazotolewa

humu zitakuwa kielelezo cha hali ilivyo katika sehemu nyingine. Ama kwa hakika kuna sehemu nyingine hapa nchini ambazo haziwezi kulinganishwa na jiji la Nairobi.

## 1.5 YALIYOANDIKWA KUHUSU SWALA HILI

Utafiti uliofanywa na Bhaiji (1976) juu ya hisia za walimu na wanafunzi kuhusu utumiaji wa Kiswahili kama lugha ya kufundishia uligundua kuwa asilimia 64 ya wanafunzi ambao walijaza hojaji hawakupendelea kubadilishwa kwa lugha ya kiingereza ili badala yake Kiswahili kitumike katika kufundishia. Idadi ya walimu nayo ilikuwa asilimia 44.

> 'Wanafunzi.......huonyesha furaha ikiwa walimu wakitumia kiingereza kama lugha ya kufundishia kwa sababu ya manufaa ambayo wale walioimarika katika lugha ya kigeni hupata katika nchi zinazoendelea'. (uk 118)[1]

Nao wazazi walionyesha hisia zao juu ya kiingereza kwa kusema:

> 'Ule mwamko wa kisiasa na kijamii ulikuwa umeendelea vizuri vijijini, na kwa hivyo tungependelea lugha ambayo wanafunzi wanaifahamu na wanaweza kuzungumza vizuri. (uk 121-122).[2]

Muganga (1977) alifanya utafiti juu ya hisia na motisha za wanafunzi wa Tanzania katika kujifunza kifaransa katika shule za upili. Kutokana na utafiti huo maswala sita yalibainika na ambayo huathiri kujifunza Kifaransa katika Tanzania.

a) Kuwa na mwelekeo mbaya wa jamii ya Kifaransa na nchi ziongeazo Kifaransa.

b) Wazazi kutowahamasisha watoto kujifunza Kifaransa.

c) Wanafunzi kutokuwa na imani na walimu wao wa Kifaransa.

d) Kifaransa (na kiingereza) kuonekana kama ni lugha za kikoloni mambo-leo na za ukengeushi.

e) Lugha hiyo haitumiki sana nchini Tanzania hata baada ya kujifunza kwa miaka 4-6, isitoshe ujuzi wa lugha hiyo hautoshi.

f) Njia za kufundishia si nzuri.

Kazi hizi mbili, za Bhaiji na Muganga, Japo zilifanywa miaka mingi iliyopita zitakuwa na manufaa mengi katika utafiti wetu. Zote zinagusia kuhusu hisia za wanafunzi katika lugha fulani.

Katika uchunguzi wa Bhaiji inabainika wazi kwamba wanafunzi wanahisi kiingereza kina manufaa mengi katika kufundishia kushida Kiswahili.

Uchunguzi wa muganga waonyesha kwamba kuna mambo kadha ambayo huathiri usomaji wa lugha fulani na hivyo kuathiri ujuzi wa mtu katika lugha hiyo.

Je, mambo haya yangalipo katika lugha ya Kiswahili? Hili ni swala muhimu kujiuliza.

Magawi,N.B. (1978) ameandika makala kuhusu shida zinazokabili ufunzaji wa Kiswahili katika shule za upili. Baadhi ya matatizo aliyoyadondoa ni kama vile:

a) Wanafunzi kukosa ari katika somo la Kiswahili,

b) Ukosefu wa vitabu mahsusi kwa somo hili,

c) Ukosefu wa walimu.

Symbo, K.(1978) anazungumzia juu ya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za upili hapa nchini Kenya.

Utafiti wa wataalam hawa wawili ulifanywa zamani sana. Wakati wa mfumo wa elimu wa 7-6-3, katika kipindi hicho somo la Kiswahili halikuwa la lazima. Bila shaka twatumaini kuweko na mabadiliko katika mfumo mpya wa elimu ya 8-4-4. Hasa kwa wakati huu ambapo somo la Kiswahili ni la lazima.
Mungania, B.G. (1986) alifanya utafiti juu ya ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili chini ya mfumo wa 8-4-4 kazi yake itakuwa yenye manufaa mengi katika utafiti wetu. Baadhi ya vipengee alivyochunguza tunanuia kuviangalia. Hata hivyo uchunguzi wake ulielekezwa katika kidato cha 1 tu. Vile vile, mfumo huo mpya wa elimu ulikuwa umeanza tu katika shule za upili.

Ziro (1987) alifanya uchunguzi juu ya 'mlinganisho wa

wa mwongozo wa Kiswahili baina ya mfumo wa elimu wa 7-6-3 na 8-4-4, kazi yake itatufaa pale ambapo tutakuwa tukichunguza silabasi ya Kiswahili chini ya mfumo wa 8-4-4.

Nabakwe N.T. (1985)alifanya utafiti juu ya vitabu vya kufundishia lugha ya Kiswahili katika kidato cha kwanza. Nia ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza iwapo vitabu kutoambatana na haja za wanafunzi hufanya somo la Kiswahili likawa kavu na kutopendeza. Katika kazi hii alichunguza vitabu vilivyotumika katika somo la Kiswahili. Haja yake ikiwa kupata sehemu zisizoambatana na haja za wanafunzi wa kidato cha 1. Vitabu viwili vilivyoonekana kupendwa sana vilikuwa ni <u>Kiswahili kwa Shule za Sekondari. kitabu cha Kwanza</u> na <u>Mafunzo ya Kiswahili, Kitabu cha Kwanza</u>.

Ikumi M.E. (1985) aliangalia vifaa vya kufundishia na kusoma katika baadhi ya shule za misingi huko tarafa ya Iventi. Katika kazi yake, alichunguza vifaa vinavyopatikana kwa kufunzia na kusoma Kiswahili, jinsi walimu wanavyochagua vifaa hivi na namna walimu na wanafunzi wanavyovitumia katika darasa.

Japo kazi ya kwanza ilichunguza vitabu vya kufundishia katika kidato cha kwanza na kazi ya pili ikachunguza vifaa vya kufundishia katika shule za msingi kazi hizi pia tumeonelea zitakuwa zenye umuhimu katika kazi yetu hasa tutakapokuwa tukichunguza swala kuhusu vifaa vya kufundisha vinavyopatikana

katika shule za upili.
Utafiti uliofanywa mwaka (1969) katika Whiteley (1974) ulionuiwa kuchunguza juu ya ufundishaji wa lugha katika shule za upili: matatizo muhimu. Kazi hii iliangalia matatizo yaliyowakumba wanafunzi na walimu kutoka kiwango kimoja cha elimu hadi kingine. Yaani kutoka shule za msingi hadi upili na kutoka shule za upili hadi kiwango cha chuo kikuu. Hivyo alichunguza uwezo wa mwanafunzi katika kiingereza na Kiswahili alipokuwa akiingia katika shule za upili.
Likhako P.I.(1991) alichunguza utoshelezaji wa Kiswahili katika kufunza hasa masomo ya kisayansi na taaluma za kiufundi. Katika utafiti wake ilibainika wazi kwamba Kiswahili kinatosheleza na kinafaa kama lugha ya kisomo.

Kazi hii yaonyesha kwamba wazo la kukidunisha Kiswahili halipaswi kuwepo kwani lugha yenyewe imejikakamua hadi kufikia kiwango cha kufundishia masomo ya kisayansi na taaluma za kiufundi.

Lakini zaidi na kuwa tunaweza kupata msamiati wa kutosha wa lugha hii. Ni maswala yapi pia yanayopaswa kuzingatiwa ili Kiswahili kama somo kiweze kuimarika ili kufikia kiwango cha kufundishia. Hili ndilo swala tunaloangalia.
Maganga C. (1978) aliandika makala kuhusu ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi, sekondari, chuo kikuu, na vyuo vya walimu. Katika kazi yake aliona madhumuni ya kufundisha Kiswahili yawe kumpa mwanafunzi uwezo wa kuitumia

lugha hiyo kikamilifu katika shughuli zote za ujenzi wa taifa lake. Kiswahili kiwe chombo asilia kinachoweza kufafanua kwa utoshelevu hekima, tabia na utamaduni wa taifa. Hali kadhalika Kiswahili kimwezeshe kudadisi bila kutumia lugha nyingineyo. Hatimaye mwanafunzi huyo awe mjenzi wa lugha ya Kiswahili.

Kazi nyingine zitakazotufaa katika tasnifu yetu ni makala yaliyoandikwa na Sultan C.I. (1976) Matatizo katika ufunzaji wa Kiswahili na Dr. A. Obura (1986) Resources for learning in language classrooms.

Tulipoziangalia kazi hizi tuliona kuwa kazi zaidi kuhusu Kiswahili katika shule za upili inahitajika kufanywa. Pia tulishawishika kuwa hadhi ya Kiswahili katika miaka hii ya themanini imebadilika. Kwa hivyo tuliamua kuchunguza Kiswahili katika za upili kwa sababu sasa ni somo la kutahiniwa katika kiwango cha shule za upili. Kwa hivyo matumaini yetu ni kuwa jambo hili litabadilisha mawazo na mitazamo ya wanafunzi.

## ..6 MSINGI WA KINADHARIA

Utafiti tunaoufanya unahusu masiala ya lugha katika elimu, hivyo tumeonelea kwamba taalum za Isimu - nafsia[3] na Isimu - jamii zitatufaa sana katika kazi yetu. Taaluma hizi mbili zimeshughulikiwa na wataalam tofauti tofauti.

Wote hawa wametumia msingi wa kinadharia kuwaongoza katika kazi zao.

Saussure (1966) akizungumzia dhana za 'langue' na 'Parole' ambazo ni sambamba na 'Competence' na 'performance' (Chomsky 1965) alijaribu kuonyesha kuwa kila mzungumzaji wa lugha huwa na ujuzi wa lugha hiyo na vile vile uwezo katika kutumia. Sifa za mtu kuijua lugha hutegemea uwezo wake wa kuitumia kwa ufasaha. Kwa hivyo mtu huenda akawa na akiba kubwa ya msamiati wa lugha yake lakini hana uwezo wa kutumia vizuri.

Katika hali halisi yaani ya kimazungumzo na kimaandishi kutoweza kuitumia lugha yake mtu kunategemea mambo tofauti tofauti kama vile mazingira yake, hisia, alizonazo kuhusu lugha hiyo, athari kutokana na lugha nyingine anazozizungumza, nafasi ya mzungumzaji katika jamii, kiwango chake cha elimu, mada anayoishughulikia na mengineo.

Katika utafiti wetu, tunanuia kuangalia mambo ambayo kwayo yanaweza kuwa vikwazo kwa mwanafunzi katika kuimudu lugha. Kuimudu lugha ikiwa na maana ya kupata ule uwezo na ujuzi katika lugha kwa mwanafunzi.

Taaluma ya lsimu-nafsia huwekea mkazo matumizi ya lugha kimawasiliano. katika taaluma hii, lengo la ufundishaji wa lugha ni kukuza kile Hymes, D. (1972) anachorejelea kama 'Communicative Competence' yaani ule ujuzi wa kuweza kutumia lugha kimuktadha.

Hatch (1982) anasema katika 'Communicative Competence'lengo kuu ni kumwezesha mwanafunzi kuwasiliana katika nyanja zote za matumizi ya lugha.

Hii yamaanisha kwamba wanafunzi wataweza kuwasiliana vizuri katika lugha ya kimaongezi, wakitumia sio tu sarufi, msamiati na matamshi yaliyo sahihi mbali pia na lugha inayokubalika katika muktadha fulani. Hili lawezekana tu iwapo wanafunzi watakuwa na ujuzi katika vipengee vifuatavyo.

a) Muundo wa lugha na msamiati.

b) Matamshi na tanakali za sauti.

Ili kupata ujuzi huu kuna mambo kadha muhimu ambayo yanapaswa kuzingatiwa katika muktadha wa shule. Kwa mfano muda wa kutosha wa kufanya mazoezi, vifaa vya kufundishia pia ni muhimu pamoja na walimu waliohitimu.

Yanayotuhusu katika taaluma hizi kwa minajili ya utafiti wetu ni (competence) ujuzi (perfomance) uwezo na (communicative competence) uwezo wa kimawasiliano.

Katika kazi yetu, tumechukulia 'competence' kama ujuzi ambao ni muhimu kwa mwanafunzi kuwa nao katika lugha.

'Perfomance' na 'Communicative Competence' hizi ni dhana mbili ambazo tumezichukulia kama ule uwezo wa mwanafunzi wa kuweza kuimudu lugha ili iweze kutekeleza wajibu wake na kwa mujibu wa utafiti wetu wajibu huu ni Kiswahili kitumike kama lugha ya mawasiliano.

Hii itawezesha lugha ya Kiswahili kuimarika zaidi.

Lakini kama tulivyodokeza hapo awali kuna masiala muhimu ambayo kwayo yanapaswa kuzingatiwa ili ujuzi huu na uwezo katika lugha uweze kukuzwa na kuimarishwa.

## 1.7 NJIA ZA UTAFITI

Kazi hii itatumia njia kadha kama mwongozo wa utafiti. Kwanza, kwa sababu ya wakati ulitolewa kwa kazi hii tumeamua kuwa na sampuli ya watu mia moja na sabini. Sampuli hii itawahusisha walimu na wanafunzi pamoja na watu kutoka wizara ya elimu.

Njia ambayo itatumika zaidi ni ile ya kutumia hojaji. Ni muhimu kutangulia kutaja kwamba, hojaji ni za aina mbili. Kuna hojaji ambayo kwa kuitumia mhojiwa anatakiwa kuyajibu maswali kwa njia ya kuandika. Pili, kuna hojaji ambayo mhojiwa anauliza maswali huku mhojaji akiyaandika majibu mwenyewe. Katika kazi hii, aina zote mbili zitatumika. Katika sampuli yetu, kuna wanafunzi ambao ndiyo watatumia aina ya kwanza ya hojaji. Aina ya pili ya hojaji itatumika zaidi na walimu pamoja na utatu kutoka ulizana ya elimu.

Maswali haya pamoja na majibu yake yanapatikana katika mwisho wa tasnifu hii. Baada ya kuchukua data tutakaa, kuifafanua na kuichanganua.

Njia ya mwisho na ambayo ni muhimu pia ni matumizi ya maktaba. Tunawajibika kutumia maktaba kusoma kazi na makala mbali mbali yanayohusiana na kazi yetu ili tuweze kuifahamu vyema zaidi.

## 1.8 NJIA ZA KUCHAGUA SAMPULI

Katika jiji la Nairobi ambako utafiti wetu ulifanyiwa, kuna idadi ya shule za upili 78.

Shule hizi zimegawanywa katika kategoria tatu. Kategoria ya kwanza ni aina ya shule za kitaifa. Kategoria ya pili ni aina ya shule za mkoa na mwisho ni kategoria ya shule za watu binafsi na za harambee.

Ikiwa utafiti wetu utachukua shule hizi zote zinazopatikana katika mji huu matatizo mengi sana yataibuka iwapo tutajaribu kuwahoji wanafunzi wote wanaopatikana katika shule hizi.

Njia iliyobaki ni ya kupata sampuli. Kwa mujibu wa kazi hii sampuli imetumika kwa maana ya sehemu ndogo ya kitu ambacho ni kiwakilisho cha kitu kikubwa. Katika uteuzi wa sampuli tulijaribu iwezekanavyo kuondoa aina yo yote ya mapendeleo ambayo yaweza kutokea.

Hatua ya kwanza tuliyofuata ili kuchagua sampuli yetu ilikuwa kuteua shule mbili kutoka kila kategoria.

Katika uteuzi wa sampuli yetu tuliamua kutumia njia ya bahati nasibu.

Shule zilizoteuliwa ni kama ifuatavyo

Shule za Kitaifa

Shule ya wavulana ya Starehe

Shule ya wasichana ya Moi Nairobi

Shule za Mkoa

Shule ya upili ya Jamhuri

shule ya wasichana Precious Blood Riruta

Shule za Watu Binafsi

Shule ya upili ya Ravals

Shule ya wavulana ya Saint Mary's

Shule za Harambee

Shauri Moyo Harmabee

Tulipata jumla ya shule saba. Hatukuweza kupata shule nyingine iliyoko katika kategoria ya shule za Harambee.

Katika shule zote tulidhamiria kupata sampuli ya wahojiwa 150. katika kila shule tulinuia kupeana jumla ya hojaji ishirini.

Ili kufanya hivi tulitumia mbinu ile ile ya bahati nasibu ili kupata wakilishi wa wanafunzi hawa.

Sampuli hiyo ya wanafunzi 20 ilichanganuliwa kama ifuatavyo. Kila kidato, kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne ilipewa

jumla ya hojaji 5.

Hizi ndizo njia zilizotumika katika kuteua sampuli yetu. Tunataraji zitatusaidia kuepukana na shida ya kuwa na wahojiwa wengi na kuwa kielelezo bora cha wanafunzi katika jiji hili.

Katika kuwahoji walimu, Tulihoji jumla ya walimu 20 ambao tuliwapata katika shule ambazo tuliwahi kutembelea.

## HAIPOTHESIA

Tulikuwa na haipothesia tatu tulipoanza utafiti huu.

Jumla ya vipindi vilivyotegewa somo la Kiswahili katika shule za upili chini ya mfumo wa 8-4-4 vinatosha.

Silabasi iliyotayarishwa kwa minajili ya shule za upili chini ya mfumo wa 8-4-4 ni pana mno.

Mbali na uhaba wa walimu waliohitimu, ukosefu wa vitabu, athari zilizoletwa na kasumba za kikoloni, ukosefu wa vifaa vya kufundishia ni miongoni mwa matatizo yanayokabili Kiswahili katika shule za upili chini ya mfumo wa 8-4-4.

TANBIHI

1. Hii ni tafsiri yetu kutoka (Bhaiji 1976: 118)

2. Tafsiri yetu (op.cit. 121-122)

3. Isimu nafsia ni tawi la taaluma ya lsimu ambalo huchunguza mtu anavyofunza lugha kwa kutumia misingi ya kisaikolojia. ji, anavyopata uwezo wa lugha?

4. Isimu jamii ni tawi la lsimu ambalo huchunguza uhusiano baina ya lugha na jamii.

Tofauti baina ya "njia za utafiti" na "njia za kuchagua Sampuli" ni ipi? Yaonekana moja ni sehemu ya nyingine!

## SURA YA PILI

### 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tutashughulikia mambo matatu muhimu. Yatakuwa ni msingi wa kuelewa matokeo na mwenendo wa uchunguzi wetu katika sura ya tatu na nne. Kwanza, tutaangalia sera ya lugha katika elimu. Tutazingatia nyakati mbali mbali za kihistoria. Tunataraji vile vile kuangalia kiswahili katika mfumo wa 8-4-4.

Sehemu ya tatu itashughulikia yale yaliyomuhimu ili kufanikisha mradi wo wote ule. Katika kazi yetu mradi huo ni kiswahili katika shule za upili.

### 2.1 SERA ZA LUGHA KATIKA ELIMU -: KABLA YA UHURU

Katika karne ya kumi na tisa, wamisheni walianza kuingia Kenya kwa kusudi la kueneza dini ya Kikristo. Licho ya kuwafunza wenyeji wa janibu hizi ukristo, wamisheni waliwapatia wafrika elimu kidogo ya kizungu. Kufikia wakati ambao Kenya ilitangazwa kuwa koloni la uingereza, makanisa ndiyo yalikuwa na jukumu la kuendesha shule hapa nchini. Serikali ya kikoloni haikujihusisha na elimu wazi wazi miaka ya mwanzo ya utawala wake. Serikali ilianza kujishughulisha na elimu mnamo mwaka wa 1911 wakati ambapo idara ya elimu ilipoanzishwa.

Baina ya mwaka wa 1911 na 1950, makanisa yakishirikiana na utawala wa kikoloni yalisimamia elimu ya wafrika kwa madhumuni

ya kutekeleza maslahi ya makundi haya mawili. Elimu hiyo mpya haikuhusishwa na mahitaji au matatizo yaliyowakabili wafrika wala utamaduni wa kiafrika. Elimu iliyotolewa na wamisheni ilinuiwa iwasaidie wafrika kujisomea Biblia ili mradi wawasaidie wamisheni hao kueneza dini katika sehemu nyingine za Kenya. Elimu iliyotolewa na wakoloni ilinuiwa kuwapa wafrika ujuzi wa kazi za makarani wa viwango vya chini katika ofisi za utawala.

Serikali ya kikoloni ndiyo iliyotoa miongozo mbali mbali ya elimu, nao wamisheni wakaitekeleza miradi hiyo. Mwongozo wa utawala wa kikoloni kuhusu elimu ulitilia mkazo maendeleo ya makundi mbali mbali katika utengano na pia katika nyanja nyinginezo za kuhudumia umma hivi kwamba kulikuwa na elimu ya wazungu, elimu ya wahindi na elimu ya wafrika. Kila mojawapo ya elimu hizi ilikuwa na madhumuni yake.

Serikali ndiyo iliyosimamia elimu ya wazungu na wahindi. Kila juhudi ilifanywa ili kuhakikisha kwamba kila mtoto wa makundi haya mawili amepata elimu iliyo bora. Elimu ya wafrika iliachiwa wamisheni kuendeleza.

Hata hivyo, wakati mwingine, serikali ilikuwa ikitoa misaada kwa makanisa ili kuyawezesha kutoa elimu kwa watoto wa Kiafrika.

Utawala wa kikoloni ulichangia nini katika kuendeleza matumizi ya Kiswahili shuleni? wamisheni walikidunisha Kiswahili hapa nchini Kenya. Tangu mwanzo, walihimiza zaidi matumizi ya lugha za kikabila. Mantiki waliyoitumia ni kwamba ni rahisi sana kuelewa fikra za mtu iwapo atatumia lugha yake ya pili, walidai kwamba ni rahisi kumfundisha mtoto katika lugha yake mwenyewe.

Baadhi ya wamisheni walipinga Kiswahili kwa madai kwamba kimefungamana zaidi na Uislamu, wamisheni walikuwa na uwezo mkubwa Kenya. Wao ndio walianzisha shule kadha na kuendelea nazo hata katika miaka ya mwanzo ya Kenya Huru. Mpaka hivi leo kuungali shule kadha zinazoendeshwa na wamisheni.

Ingawa wamisheni walisaidia kukuza Kiswahili kwani waliwajibika kufanya hivyo, (kwa mfano, iliwalazimu kutafsiri Biblia katika Kiswahili.) Lakini walipendelea zaidi matumizi ya lugha za kikabila. Wanafunzi wengi wa nyakati hizo waliimarika katika matumizi ya lugha za kikabila, kiingereza na mwisho wakawa na ujuzi mdogo sana wa lugha ya Kiswahili. Kwa wakati, huu wamisheni walisisitiza zaidi matumizi ya kingereza katika shule.

Matumizi ya Kiswahili vile vile yalitatizwa na mawazo kwamba Kiswahili ni lugha ya 'Kisetla'[2] wakoloni walidai kuwa Kiswahili ni lugha ya kusemwa na 'maboi'[3]. Kutokana na madai haya, wakikuyu walianzisha vyama. Vyama hivi vilikuwa ni 'Kikuyu Independent School Association' na 'Kikuyu Karinga School Association'.

Vyama hivi vilipinga matumizi ya Kiswahili kuligana na jinsi ambavyo kilikuwa kikitumiwa kuwadharau wafrika. Badala yake walihimiza matumizi ya kiingereza katika shule zao. Jambo hili liliathiri sana matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kiingereza kwa mara nyingine tena kikawa cha kutukuzwa na kupewa hadhi hata na wafrika wenyewe. Matokeo yake ni kwamba mpaka sasa kiingereza kinajivunia hadhi hii ya juu ambapo Kiswahili kingalijaribu kujiinua. Maoni yetu ni kwamba mambo haya yana athari zake mpaka leo. Hadi sasa yaelekea kana kwamba ufundishaji wa lugha ya kiingereza huwekewa mkazo zaidi ya ufundishaji wa lugha ya kiswahili. Vile vile matumizi ya lugha ya kiingereza hutiliwa mkazo katika shule kuliko Kiswahili.

Serikali ya kikoloni nayo iliendesha siasa zake za ubaguzi kwa kuweka matabaka ya kikabila. Katika elimu kulikuwa na shule mbali mbali za kikabila, na mitihani ya kuingilia shule za Sekondari ilikuwa mitatu. Katika shule hizi Kiswahili kilifundishwa katika shule za Kiafrika (na kiarabu) peke yake.

Tume baada ya tume zilizoanza kuchaguliwa tokea mwaka wa 1919 hadi kukaribia mwaka wa kupatikana uhuru, 1963, ili kuchungua masiala ya ardhi, idadi ya watu, siasa, uchumi na elimu - zilikuwa zikipinga matumizi ya Kiswahili isipokuwa pale ambapo hapakuwa na budi.

Tume ya Taalimu katika Mahamia ya Afrika ya Mashariki, ya mwaka wa 1919, ilipendekeza kuwa mafunzo ya madarasa ya chini yaendeshwe kwa lugha za kikabila, kiingereza kifunzwe katika shule zote za kienyeji.

Kuhusu Kiswahili ilitoa maoni kuwa Kiswahili ni 'lugha ya Kigeni' kwa tajiri na mwajiriwa na kwamba ikiwa kwatakikana kufunzwe lugha ya kigeni basi lugha hiyo iwe ni Kiingereza.

Yaelekea kwamba dhamira ya kutoa maoni kama haya kuhusu Kiswahili ilikuwa ni 'kukipaka tope' ile wenyeji wakidharau.

Tume ya Phelps-Stokes ya 1924 ilitaka lugha ya Kiswahili, Kikuyu, Kiluo na Kibaluhya zikubaliwe kuwa ndizo lugha kubwa za kwanza za kufundishia na kwamba kiingereza kisomeshwe kuwa ni lugha ya pili hata katika shule za vijijini. Lakini Kiswahili kisifunzwe ila katika shule za pwani tu.

Taarifa ya Tume ya Afrika Mashariki ya 1925 ilitoa maoni yaliyoshabihiana na ya tume ya 1919, yaani madarasa ya chini yafunzwe kwa lugha za kikabila na hapo baadaye kufunzwe kwa lugha ya kiingereza. Na kukasisitizwa kwamba wakati kiingereza kinapofunzwa kifunzwe kwa kikamilifu.

Tume hizi zote zilipendekeza mafunzo yatolewe kwa lugha za kikabila na kusisitiza mafunzo ya kiingereza yatolewe kwa kidhati.

Kiswahili kiliendelea kudidimizwa. Wanafunzi waliokuwa wakifuzu katika shule na vyuo mbali mbali wakawa wameimarika katika matumizi ya kiingereza na kupata ujuzi hafifu sana wa Kiswahili.

Mwaka wa 1928, Halmashauri ya Hilton Young ilitoa pendekezo kwamba Kiswahili kifunzwe kama lingua franka na polepole kiingereza kitumike. Mnamo mwaka wa 1929, mengi yalifanywa kuhusu sera ya lugha hapa nchini Kenya. Wakurugenzi wa elimu wa Afrika Mashariki na Kati walikuwa na mjadala mkali kuhusu kukifanya Kiswahili lugha ya kufunzia. Mapendekezo yao yalikuwa: Lugha za kikabila zitumike kwanza katika kufunzia. Baadaye Kiswahili kitumike na pale ambapo pana lugha kuu, kiingereza kisitumike mpaka hapo baadaye.

Kwa wakati huu wamisheni walipendelea kutumia Kiswahili kama lugha yao ya kufunzia. Hata hivyo mkurugenzi wa elimu mara kwa mara aliwakumbusha kwamba nia ya serikali iwe kukifanya kiingereza Lingua Franka Ya Afrika Mashariki. Masetla nao walipinga kiingereza kisifunzwe kamwe. Kwa mfano, Major E.S. Grogan hakuweza kufikiri tukio la hatari zaidi 'kuliko sisi (wazungu) kuwafundisha lugha hii (kiingereza) watu (wafrika) wengi ambao elimu yao ya kufaa ni kufanya kazi mashambani'[4].

Yaelekea kwamba katika nyakati hizi mbili, matumizi ya Kiswahili yalihimizwa. Hii ilikuwa ni hatua madhubuti katika uenezaji wa Kiswahili kama Lingua Franka. Lakini pamoja na hayo yaonekana kuwa kule kukipandisha Kiswahili hadhi kulikuwa na sababu zake, kama tulivyokwisha kusema wamisheni na wakoloni walikuwa na matakwa yao waliyotaka yatekelezwe na wafrika, pili walihofia kwamba kuwafunza wafrika kiingereza ni sawa na kuwapa chombo cha kisiasa. Yaani iwapo wafrika wangefahamu kiingereza, wangeweza kusoma fasihi kama ya U-maksi na hivyo kuwachochea kujikomboa kutokana na utawala wa wazungu (waingereza)

Mnamo mwaka wa 1942, kamati chini ya mwenyeketi L.J. Beecher iliteuliwa. Kamati hii iliteuliwa ili kuchunguza swala kuhusu ufundishaji wa lugha katika shule za wafrika. Kamati hii ilipendekeza matumizi ya lugha za kikabila. Vile vile kamati hii ilipendekeza kwamba, kiingereza kichukue nafasi ya Kiswahili kama lingua franka ya Kenya kwa wakati mchache kama iwezekanavyo.

Kamati ya Beecher ya mwaka wa 1949 ilipendekeza kwamba lugha ya kufunzia iwe kiingereza. Kiswahili kitumike kama lugha ya kufunzia katika miji na vitongoji vyake. Sehemu za mashambani zitumie lugha za kikabila katika viwango vya chini baadaye Kiswahili kitumike.

Hadi sasa tunaona utawala wa kikoloni ukihimiza matumizi ya lugha za kikabila. Hata hivyo tukichunguza kwa makini twaweza kujiuliza iwapo kungekuwa na uwezekano wa kutoa vitabu katika lugha za kwanza, pili yaonekana wazi kwamba muda mwingi sana ungetumika katika kufasiri vitabu katika lugha ya kwanza. Isitoshe, kuna uwezekano kwamba wangekabiliwa na matatizo ya tahajia.

Hata hivyo tunaelezwa kwamba baada ya juhudi hizo zote za kuhimiza matumizi ya lugha za kwanza na kujaribu kuchapisha vitabu katika lugha hizo, kufikia mwaka wa 1950 ilikuwa imechapisha vitabu 64, 21 ikiwa katika lugha za kikabila za Kenya (Kikuyu, Luo Luhya, Meru na Kikamba) na 23 ikiwa ni katika lugha ya Kiswahili. Hivyo yabainika wazi kwamba japo Kiswahili kilikuwa kikidunishwa lakini haja ya vitabu vya Kiswahili ilikuwa kubwa kushida vitabu vya lugha za kwanza (Kikabila).

Mwaka wa 1953, Tume ya Kifalme ya Afrika Mashariki, ilipendekeza kiingereza kianze kufundishwa katika madarasa ya chini katika shule za msingi. Tume hii pia ilitoa madai kwamba kukifundisha Kiswahili ili kiwe lugha ya pili ni kupoteza wakati bure. (East African Royal Commission).

Kwa mara nyingine tena, walimu wengi zaidi wakafunzwa mipango ya kufundishia kiingereza, na mwaka 1957 kukaanzishwa makao maalum ya kuchagua na kuhimiza matumizi ya kiingereza.

Lakini pamoja na hayo, ni watu wengi ambao bado hawawezi kujivunia uwezo wao katika lugha hii. Lakini karibu kila mtu nchini Kenya ana uwezo fulani ingawa kwa kiasi Kidogo katika lugha ya Kiswahili.

Katika mwaka wa 1961, mitihani ya kuingilia shule za Sekondari ya K.A.P.E. (Kenya African Preliminary Examination) iliyofanywa katika lugha za kikabila iliyondolewa. Badala yake kulianzishwa mtihani wa C.P.E. (Certificate of Primary Education) uliotungwa kwa kiingereza ili kuhudumia makabila yote. Awali Kiswahili kilikuwa ni somo la kutahiniwa katika shule za Kiafrika, lakini katika mtihani huu mpya, kikawa hakitahiniwi tena. Hivyo siasa ya kukitukuza kingereza ikawa inatekelezwa kwa ukamilifu. Pamoja na hayo siasa hiyo haikufanikiwa kama wenyewe wazungu walivyotaka. Kwani kwanza, pamoja na juhudi zote hizo za kukiondoa Kiswahili katika matumizi, kukawa na shule kadha zilizohitaji Kiswahili, pili, haja ya vitabu vya Kiswahili haikufifia. Kiingereza nacho, pamoja na huduma na hasara zote, kilikuwa hakijafika kiwango cha kudai kuwa ndiyo lugha ya umma wa Kenya.

Hadi hii leo Kiswahili ndicho kinachoendelea kushika cheo hicho. Hata katika shule za msingi pia, matokeo ya wanafunzi ya kiwango cha kufahamu kusoma kingereza hayakuwa mazuri; maana baada ya juhudi za miaka saba hiyo bado kukawa kunatokea wanafunzi ambao kiwango chao kilikuwa ni cha chini sana.

Hivyo katika mfumo wa utawala wa kikoloni tunaona Kiswahili kikidunishwa na kutopewa nafasi ya kujitambulisha. Hata hivyo Kiswahili hakikubali kuzama bali kiliendelea kukua na kuenea katika taifa la Kenya.

Jambo muhimu ambalo twapaswa kugusia ni kwamba hizi ndizo sera ambazo Kenya ilijipata nazo wakati wa kujipatia uhuru. Ni sera ambazo hazikutilia maanani lugha ya Kiswahili.

## 2.2 SERA ZA LUGHA KATIKA ELIMU-: BAADA YA UHURU

Baada ya Kenya kujipatia uhuru mwaka wa 1963, mipango ya kukistawisha kiingereza iliendelea hata ingawa matumizi ya Kiswahili yalizidi kuongezeka. Serikali ya Kenya huru haikuonekana kuweka misingi yake kuhusu sera za lugha tangu mwanzo.

Wasomi waliochukua hatamu za uongozi walikuwa hawakitilii maanani Kiswahili. Juhudi zao zikawa zinaelekezwa kwenye kukitukuza na kukipa hadhi kiingereza. Hii ni kutokana na ujuzi wao hafifu wa lugha ya Kiswahili, pamoja na hayo walikuwa wamepitia mfumo wa elimu wa kikoloni ambao ulionekana kukitukuza kiingereza huku ukikidunisha Kiswahili.

Tume ya elimu ya Kenya Ominde, (1964) ndiyo ilikuwa ya kwanza Kenya huru kushughulikia swala la elimu. Mapendekezo yake yalikuwa kwamba kiingereza kiendelee kutumiwa kufundishia katika shule za msingi tokea darasa la kwanza, vile vile lugha za

kikabila zitumiwe kufundishia lakini ikaonelea si vibaya kuwa na kipindi kimoja kila siku cha kutoa ngano, kuhusu Kiswahili mapendekezo yalikuwa kwamba matumizi ya Kiswahili yapenuliwe kwa sababu-:

1) Kama chombo cha ziada cha kiafrika cha kuunganisha na kuleta umoja.

2) Kama chombo cho kutilia nguvu mawasiliano baina ya nchi za Afrika Mashariki, Zaire na Afrika ya Kati.

Kiswahili kikapendekezwa kuwa somo la lazima katika shule za msingi kuanzia kiwango cha chini kama iwezekanavyo, Kiswahili chaonekana kuchukua nafasi ya mwisho katika mapendekezo ya tume hii. Hakikupewa nafasi maalum tangu mwanzo.

Haya yote ni matokeo ya kasumba za kikoloni. Kenya huru iliendelea kukididimiza Kiswahili huku ikihimiza matumizi ya kiingereza katika shule. Maendeleo yaliyopatikana kuhusu Kiswahili yaonekana yakitokana na juhudi za watu kuliko juhudi za serikali katika kukijengea msingi bora.

Ripoti ya Prator-Hutasoit ya mwaka 1965 ilipendekeza mfumo mpya katika shule za msingi. Jukumu la mfumo huu lilikuwa kutumia kiingereza kama chombo cha kufundishia kuanzia darasa la kwanza katika shule za msingi. Matokeo yalikuwa kwamba somo la kiingereza liliimarika zaidi na kuziletea hasara lugha za kikabila na kwa upungufu kidogo, Kiswahili.

Takriban ripoti zote hizi zilipendekeza juhudi za kukiendeleza kiingereza katika shule na kutaraji kwamba Kiswahili kingekua bila kuwekewa juhudi zo zote. Katika shule za sekondari kiingereza kilipewa vipindi saba au vinane. Kwa juma moja ilhali Kiswahili kilipewa vipindi visivyozidi vinne. Kadhalika katika shule yenye walimu tuseme 26 hivi, walimu wa Kiswahili walikuwa hawazidi wawili wa walimu wa kiingereza sita; walimu waliobaki walitumia kiingereza katika kufundishia masomo haya mengine. Jambo hili lingali laendelea katika Kenya huru.

Yaelekea kwamba, ingawa shughuli za kukiendeleza Kiswahili katika shule hazina mpango maalum na ingawa kinadidimizwa namna hiyo lakini Kiswahili hakikubali kuzama bali huibuka tena.

Aliyekuwa waziri wa elimu mwaka wa 1967, Bwana Jeremiah Nyagah alitangaza kuwa Kiswahili kingefanywa somo la lazima katika viwango vya kielimu hadi vyuo vya walimu. Alitoa maoni kuwa:

> Kiswahili kitakuwa somo la lazima katika shule za sekondari ikiwa twataka tuwe wamoja, na wa taifa moja, katika wakati mchache. Mawasiliana katika lugha hii ni kiungo muhimu, kwa sababu lugha za kikabila ni nyingi mno na kiingereza kinasemwa na kufahamiwa na wachache sana.

Uamuzi wake ulitatizwa na ukosefu wa walimu wa kutosha waliofuzu kufundisha somo hili.

Wakati wa mapendekezo haya, kulikuwa na kazi chache za Kiswahili; ukosefu wa vitabu vinavyofaa katika viwango mbali mbali pia ulitatiza mpango huo.

Wanafunzi wakawa na hisi kwamba somo hili ni duni likilinganishwa na masomo mengine. Hizi ni baadhi ya hisi ambazo mpaka sasa zapatikana miongoni mwa wazazi fulani na wanafunzi. Ni hisi zinazokidunisha Kiswahili. Pendekezo la waziri, ingawa lilikuwa na nia nzuri hayakuweza kufaulu.

Pamoja na kuwa matamshi kama haya yamepata kutolewa Kenya na watu wenye madaraka katika elimu lakini Kiswahili kimefanyiwa juhudi ndogo kabisa ukilinganisha na juhudi zinazofanywa kukipeleka mbele kiingereza. Yaelekea kwamba zile 'mbegu zilizopandwa na kupaliliwa' wakati wa utawala wa kikoloni, sasa zimechipukiza na kustawi hasa tokea uhuru kupatikana.Katika mtihani wa kidato cha nne 'East African Certificate of Education' ambao ulibadilishwa na kuwa 'Kenya Cetificate of School Education.' Mwaka wa 1984, mwanafunzi alihitajika kufanya na kutahiniwa katika somo la kiingereza lakini somo la Kiswahili halikuwa la lazima.

Jambo muhimu kuhusu sera tangu uhuru ni kwamba Kiswahili kimetukuzwa. Lakini, mipango ya kutekeleza sera yenyewe ndiyo haijaimarika kabisa. Iwapo Kenya itajivunia ufanisi katika lugha ya Kiswahili, serikali inawajibika kujitolea zaidi kuweka wazi sera za lugha na shughuli zote za Kiswahili.

Hata hivyo hivi karibuni kumetokea hatua za kuridhisha katika juhudi za serikali za kukisambaza Kiswahili. Kufuatia kuanzishwa kwa mfumo wa elimu wa 8-4-4, Kiswahili ni somo la lazima kuanzia darasa la kwanza katika shule za msingi. Ni somo la kutahiniwa katika mtihani wa mwisho wa masomo ya msingi.

Pili, katika taratibu mpya za mtihani wa kidato cha nne, katika mfumo huu 'lugha ya Kiswahili' pamoja na 'fasihi ya Kiswahili' ni masomo ya lazima na ya kutahiniwa kwa kila mwanafunzi. Hii ni hatua muhimu sana katika kukikuza Kiswahili.

Tatu, Kiswahili sasa ni somo la lazima kwa wanafunzi wa vyuo vya walimu wa shule za msingi kote nchini.

Ingawa serkali imejitahidi hivyo, bado kuna matatizo yanayokumba somo hili. Kwa mfano, hakuna walimu wa kutosha wa kufundisha somo hili. Vile vile kuna upungufu wa vitabu. Iwapo serikali itafaulu katika juhudi zake, basi ni muhimu kupeleka watu zaidi katika kozi au semina fupi ili waweze kufundisha somo hili.

Maoni yetu ni kuwa kwa kufanya hivyo hadhi ya Kiswahili itaweza kuinuka hapa nchini Kenya. Pamoja na hayo wanafunzi watajifunza somo hili kwa unyeti zaidi.

Ijapokuwa Kiswahili nchini Kenya kilitambuliwa kuwa na sifa zote za kuwa lugha ya taifa mwaka wa 1969 na kutangazwa kuwa lugha ya taifa mwaka wa 1974, hatua madhubuti hazijachukuliwa kukikuza na kukipatia cheo kinachostahiki.

Bado kuna wengi kati ya umma wa Kenya, wazee kwa vijana ambao hawakithamini. Jambo hili limesababishwa na sababu kadha. Lakini, swala kubwa ni la kisaikolojia linatokana na hisia za watu kuhusu Kiswahili. Wengi wanaiona kama lugha ya mazungumzo ambayo haiwezi kujitosheleza katika uandishi. Wengine wanaidharau kwa sababu haina sifa na utukufu ambao lugha kama kiingereza hujivunia. Haya yote ni matokeo ya kasumba ya ukoloni au ukoloni mambo - leo. Kenya haijajaribu kujikomboa na hali ilivyoachwa na mkoloni. Kabla ya kufa kwake Raisi Jomo Kenyatta alikuwa ametoa wito kwamba Kiswahili kiwe lugha ya bunge (Daily Nation, 4th July 1974). Jambo hili lilirekebishwa hata katika katiba lakini punde baada ya kifo chake, jambo hili lilibadilika na wabunge wakapewa uhuru wa kuzungumza Kiswahili au kiingereza bungeni (Mkangi 1985)

## 2:3 KISWAHILI KATIKA MFUMO WA 8-4-4

Elimu ni nyanja mojawapo inayoweza kutumika katika kuendeleza lugha. Ni katika elimu ambapo msamiati zaidi waweza kuzalishwa ili kutumika. Katika kufunzia, makamusi maalum ya taaluma mbali mbali yaweza kuundwa ili kusaidia katika kisomo. Na kwa njia hii lugha hiyo itaendelezwa.

Mfumo wa elimu wa 8-4-4 ulipendekezwa na kamati ya Machkay mnamo machi 1982; wizara ya elimu ilianzisha mfumo huu mwaka wa 1985. Mfumo huu wa elimu unatilia mkazo masomo ya kiufundi. Hili ni jambo ambalo halikusisitizwa na mfumo wa hapo awali wa 7-6-3.

Kuhusu lugha, kufikia mwaka wa 1985, mfumo wa elimu wa 8-4-4 ulipoanzishwa ni kiingereza tu kilichokuwa somo la lazima na la kutahiniwa katika shule za msingi na shule za upili Kiswahili hakikuwa somo la lazima wala la kutahiniwa katika viwango vyote vya elimu.

Katika shule za upili, Kiswahili kilipewa idadi ya vipindi vinne kila wiki huku kiingereza kikipewa idadi ya vipindi sita au saba kwa juma moja. Katika shule nyingi za msingi, japo Kiswahili kiliwekwa kwenye ratiba ya masomo, lakini walimu wengi walitumia wakati huo kusomesha masoma mengine yaliyokuwa yakitahiniwa. Katika mfumo wa elimu 8-4-4, somo la Kiswahili ni la lazima katika shule za msingi na sekondari. Vile vile somo hili linatahiniwa mwishoni mwa masomo ya darasa la nane na kidato cha nne. Hii yamaanisha kwamba Kiswahili kimewekwa katika kundi moja na masomo mengine yanayorahisisha mawasiliano kama kiingereza.

Maoni yetu ni kwamba, kule kukifanya Kiswahili somo la lazima kutainua hadhi ya somo hili. Hali ile ya zamani ya kukifanya Kiswahili kiwe ni somo la hiyari ilikuwa inakifanya Kiswahili kivie na kudunishwa, kiasi kwamba kilinyimwa haki yake ya kukua na kuzangaa (hasa tujuapo kwambo Kiswahili ni lugha ya taifa).

Tukirejelea mapendekezo ya kamati ya Mackay kwa ambavyo ilivyoshughulikia Kiswahili twaona kwamba kamati hiyo ilipendekeza kuanzishwa kwa kitivo cha taaluma ya jamii, utamaduni na maendeleo ambacho kingefundisha lugha za kiafrika ikiwepo lugha ya Kiswahili na lugha nyinginezo za Kenya.

Katika ibara ya 133 ya ripoti yake, kamati hii ilisema:

> Taaluma ya Kiswahili na masomo ya maendeleo yanahitaji kutiliwa mkazo. Ingawa Kiswahili ndiyo lugha ya taifa, kunao vijana wengi waliohitimu masomo ya chuo kikuu ambao hawawezi kuwasiliana kwa Kiswahili. Kutokana na hayo, kamati ya uchunguzi inapendekeza kuwa Kiswahili kifanywe kuwa somo la lazima katika chuo kikuu cha pili (uk.43)

Kamati hiyo iliendelea kueleza kwamba:

> '....imepokea mapendekezo mengi yanayopendekeza kwamba Kiswahili na lugha nyingine za Kenya zitiliwe mkazo zaidi katika kiwango cha chuo kikuu kuliko ilivyo sasa......kamati inaonelea kwamba idara au hata taasisi ya kushughulikia utafiti wa lugha za Kiafrika haina budi kuanzishwa humu nchini'. (uk.44)

Kiswahili kitatiliwa mkazo vipi katika shule za upili? Kama tulivyokwishaona masomo ya 'fasihi ya Kiswahili' na 'lugha ya Kiswahili' yameunganishwa pamoja na kuwa somo moja la Kiswahili.

Vipindi vya somo la Kiswahili katika ratiba za shule imepungua. Hapo awali, lugha ya Kiswahili ilikuwa imepangiwa vipindi vinne kwa juma nzima, nayo fasihi ikapewa vipindi vitatu kwa kila juma.

Hivyo jumla ya vipindi vya somo la Kiswahili vilikuwa ni saba. Katika mfumo wa 8-4-4 jumla ya vipindi vya Kiswahili ni tano kwa kila juma. Ingawa kuna upungufu wa vipindi viwili kila wiki, jambo hili limesababishwa na wingi wa masomo katika mfumo huu wa 8-4-4. Hata hivyo, jambo la kusikitisha ni kwamba somo la kiingereza limeongezewa vipindi na kuwa vinane baada ya ukaguzi mpya wa mfuo wa 8-4-4.

Haijulikani ni kipimo kipi kilichotumiwa ili kuongezea somo la kiingereza vipindi huku Kiswahili kikibaki na vipindi vitano. Yaonekana kwamba ile kasumba ya kikoloni, ya kukiona kiingereza kama lugha bora ikilinganishwa na Kiswahili haijadidimia.

Hata hivyo, mfumo wa 8-4-4 kwa kiwango fulani umeanza kubadilisha fikira na mitazamo ya watu kuhusu lugha ya Kiswahili. Vitabu vingi vimechapishwa ili kuweza kukimu mahitaji ya kufunzwa kwa lugha hii katika shule za msingi na za upili. Vitabu hivi vyote hatuwezi kusema kwamba vinafaa lakini ni hatua muhimu katika maendeleo ya Kiswahili hapa nchini Kenya.

## 2.4 VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA WALIMU

Ili kuhakikisha kuwa mradi wo wote unafaulu, ni sharti mambo kadha yatimizwe. Kwa mfano, ili kuhakikisha kwamba mfumo wa elimu wa 8-4-4 unafaulu, kuna mambo yanayopaswa kuzingatiwa. Mambo haya yanahusu ujenzi wa karakana na maabara katika shule zote hapa nchini.

Kila somo katika shule za upili litahitaji vifaa vya kufundishia vya kutosha, kama vitabu, silabasi, miongozo itakayotumiwa na walimu pamoja na ratiba za masomo kwa kila somo.

Kazi hii imekuwa ikitekelezwa na Taasisi ya elimu ya Kenya (K.I.E.). Taasisi hii huwa na idara mbali mbali kwa kila somo. Idara hizi ndizo hutayarisha silabasi, miongozo ya kufundishia pamoja na kupendekeza vitabu vitakavyotumiwa katika somo.

Tayari idara ya Kiswahili katika Taasisi hii imefanya mengi kuhusu ufundishaji wa Kiswahili katika mfumo wa 8-4-4 wafaulu. Baadhi ya mambo ambayo wamekwisha kutekeleza ni kutoa silabasi ambazo zinatumiwa shuleni pamoja na kupendekeza vitabu mbali mbali ambavyo vinafaa kutumiwa katika kufundisha. Swala la walimu, ni muhimu sana kuzingatiwa ili kufanikisha somo la Kiswahili katika shule za upili. Kama tulivyokwisha kudokeza hapo awali somo hili halikuwa la lazima katika mfumo wa elimu wa hapo zamani.

Lakini, katika majilio ya mfumo mpya wa 8-4-4, Kiswahili sasa ni somo la lazima swala ambalo twapaswa kujiuliza ni je, kuna walimu wa kutosha wa kufundisha somo hili? Ni kweli kwamba, kwa muda mrefu hapa nchini Kenya, kumekuwa na upungufu wa walimu wa Kiswahili. Ili kukabiliana na tatizo hili, Taasisi ya elimu ya Kenya ikishirikiana na idara ya ukaguzi katika wizara ya elimu zimekuwa zikitayarisha mara kwa mara ili kufahamisha tofauti za kitaalum na mabadiliko mbali mbali yanayojitokeza katika somo la Kiswahili.

Ufundishaji wa somo lo lote lile hauwezi kufanikiwa bila kuwahusisha wakaguzi wa elimu. Wakaguzi hawa huwaongoza walimu po pote pale wanapokwenda tenge katika ufundishaji. Hivyo, Kiswahili huwa na wakaguzi ambao wameteuliwa na wizara ya elimu. Hata hivyo, wakaguzi hawa wanapotembelea shule fulani huhisiwa na walimu kuwa kama wapelelezi, ambao haja yao kubwa si kuwashauri walimu bali ni kuwakosoa na kuwashutumu kwa kazi ambayo wamekwisha kutekeleza. Hili ni jambo ambalo linapaswa kurekebishwa.

## 2.5 HITIMISHO

Kwa hayo, tumejaribu kuonyesha kwamba kule kudidimizwa na kudunishwa kwa Kiswahili hapa nchini Kenya kuna misingi yake katika historia. Sera za lugha katika elimu, kabla na baada ya uhuru zilikidhalalisha Kiswahili. Hisia kwamba Kiswahili si somo la muhimu zatokana na zile kasumba za kikoloni. Watu waliopitia mfumo wa kielimu wa kikoloni ndio walijikuta na vyeo katika serikali huru ya Kenya. Ni kutokana na ujuzi wao hafifu wa lugha ya Kiswahili ambapo Kiswahili kiliendelea kupingwa. Hata hivyo Kiswahili hakikubali kuzama bali huendelea kukua na kusambaa bila ya juhudi zo zote. Hivi sasa, Kiswahili ni somo la lazima katika shule za msingi na za upili. Ni matumanini yetu kwamba katika siku za usoni Kiswahili kitaweza kutumika kama lugha ya kisomo kwa baadhi ya masomo hapa nchini Kenya. Tayari nchi kama Tanzania hutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya kisomo.

## TANBIHI

1. Oliver, R. (1952): The missionary factor in E. Afrika, Longman, London (uk. 22-23).

2. 'Kisetla:' Ni lugha ilivyotumiwa kisegemnenge na walowezi na masetla kuwakejeli wafanyakazi waafrika.

3. 'Maboi:' Ni watumishi wa kiafrika nyumbani na mashambani ya wazungu na pia wahindi.

4. Majadiliano ya Baraza la kutunga sheria Oktoba 18, 1929, kutokana na makala ya Tom Gorman, 'Development of Language Policy In Kenya', yaliyomo katika kitabu Language In Kenya, (mhariri, W.H. whitely), O.U.P., Nairobi, 1974.

SURA YA TATU

## 3.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tutashughulikia matokeo ya utafiti wetu. Matokeo haya tutayapanga kuligana na maswala mbali mbali yaliyojitokeza katika hojaji yetu. Tulikuwa na hojaji za aina mbili. Aina ya kwanza ya hojaji ilikuwa imelengwa kwa walimu na aina ya pili ya hojaji ikalengwa kwa wanafunzi.

Hojaji tulizotayarisha ziliwajibika kumwelekeza mhojiwa katika kutoa maoni mbali mbali kuhusu vipengele ambavyo tunachunguza.

Sehemu ya kwanza ya hojaji yetu ilinuia kuchunguza ratiba za masomo na kulinganisha idadi ya vipindi vilivyotengewa Kiswahili dhidi ya masomo mengine. Jambo hili lingetuwezesha vile vile kuchanganua umuhimu unaopewa somo la Kiswahili.

Kuhusiana na vifaa vya kufundishia tulitaka kuchunguza iwapo walimu hupata vifaa hivi kutoka kwa Taasisi ya elimu hapa Kenya (Kenya Institute of Education).

Sehemu ya tatu ya hojaji ilitupasa tupitie silabasi iliyotolewa kwa madhumuni ya Kiswahili katika mfumo wa 8-4-4.

Sehemu ya nne ya kazi yetu ilichunguza hisia za wanafunzi juu ya Kiswahili katika mfumo wa 8-4-4.

Mwisho tulitaraji kupata maoni, mapendekezo au mashauri yo yote ya wahojiwa kuhusu somo la Kiswahili katika shule za upili.

## 3.1 MATOKEO YA HOJAJI

Katika sehemu hii, kwanza tunaonyesha jinsi wahojiwa walivyojitokeza kuhusiana na vipengele mbali mbali tulivyotaja awali. Kipengele cha kwanza kinahusiana na shule za wahojiwa. Shule zenyewe tulizipanga katika kategoria nne.

JEDWALI LIFUATALO LAONYESHA AINA ZA SHULE

| AINA YA SHULE | IDADI YA SHULE | IDADI YA WANAFUNZI |
|---|---|---|
| Shule za kitaifa | 2 | 40 |
| Shule za mkoa | 2 | 40 |
| Shule za watu binafsi | 2 | 40 |
| Shule za Harambee | 1 | 30 |
| JUMLA | 7 | 150 |

JEDWALI LA 1

Idadi ya wanafunzi waliohojiwa ilikuwa ni 150. Katika kila kategoria tulichukuwa idadi ya wanafunzi 40. Ni kategoria ya shule za Harambee tu ambapo tulichukua idadi ya wanafunzi 30. Upungufu huu ulisababishwa na ukosefu wa shule za Harambee katika jiji la Nairobi. Tulifanikiwa kupata shule moja tu ya aina hii.

KIWANGO CHA ELIMU CHA WANAFUNZI

Kuhusu viwango vya elimu vya wanafunzi wote, tulichukua viwango vyote vya shule za upili.

Hivyo tulichukua kidato cha kwanza hadi cha nne. Jedwali kuhusu kipengele hiki yapatikana katika kiongezo (Appendix)

## 3.2 UGUNDUZI WA UTAFITI HUU

### 3.2.1 MGAWO WA VIPINDI VYA KISWAHILI

Hapo awali, vipindi vilivyotengewa 'lugha ya Kiswahili' vilikuwa vinne. 'Fasihi ya Kiswahili' ilitengewa vipindi vitatu. Kwa jumla somo la Kiswahili lilikuwa na vipindi 7. Walakini kufuatia kuunganishwa kwa masomo haya mawili lugha na 'Fasihi ya Kiswahili' vipindi hivi vilipungua na kuwa vitano kila juma. Upungufu huu umesababishwa na ongezeko la masomo katika mfumo wa 8-4-4. Hata hivyo kiingereza kimepewa jumla ya vipindi vinane kwa kila juma.

Kati ya wanafunzi 150, ni wanafunzi 118 (79%) ambao walidai kwamba somo la Kiswahili linapaswa kuwa na idadi sawa ya vipindi na kiingereza. Ni wanafunzi 15 pekee (10%) ambmo walidai kwamba somo la Kiswahili linapewa muda mwingi.

Tulipowahoji walimu kuhusiana na swala hili kati ya walimu 20, ni walimu 7 (35%) walionelea kwamba vipindi vilivyogawiwa somo la Kiswahili vinatosha, hawa waliosema kwamba idadi ya vipindi vinatosha baada ya kuwahoji zaidi tuliona kwamba wengi wao wanatoka katika shule za watu binafsi na Harambee. Walimu watatu kati yao walisema kwamba wana jumla ya vipindi 30 kwa kila juma.

Kwa hakika walimu hawa hawana muda wa kutosha wa kutayarisha kazi yao vizuri. Pamoja na hayo, walimu wengi walilalamika kwamba Kiswahili hakipewi umuhimu wa kutosha. Walidai kwamba kiingereza kingali kinapewa umuhimu kushida Kiswahili kwa kugawiwa vipindi vinane kila wiki huku Kiswahili kikigawiwa vitano.

Yaonekana kwamba hata wanafunzi wameanza kuona umuhimu wa somo la Kiswahili. Katika hojaji, wengi walionelea kwamba somo la Kiswahili halipewi muda wa kutosha. Pili, wengi waliona kwamba somo la Kiswahili linafaa kupewa muda sawa na somo la kiingereza. Hii ni hatua madhubuti kwa Kiswahili.

Hata ingawa Kiswahili kimefanywa kuwa somo la lazima katika mfumo wa 8-4-4 ile mantiki ya kukiona kiingereza kama lugha bora ikilinganishwa na kiswahili haijafutika kabisa miongoni mwa watu hapa nchini Kenya. Kule kukipa somo la kiingereza vipindi vingi linathibitisha kauli hii. Lakini kama tulivyotangulia kusema katika sura ya pili, Kiswahili hakikubali kuzama bali huendelea kukua na kusambaa.

## 3.2.2 VIFAA VYA KUFUNDISHIA

Vifaa vinavyotumiwa na walimu wa Kiswahili ni pamoja na vitabu na vifaa vinginevyo kama Radio, chati na michoro ambavyo vinawezesha wanafunzi kuelewa zaidi wafunzwayo.

Claessan (1988) anasema kwamba mwanafunzi huweza kuhifadhi asilimia 60 ya jambo analofunzwa kwa kuona (yaani kwa matumizi ya vifaa) na huweza kukumbuka asilimia 40 tu ya jambo analofunzwa bila kuona. Hivyo vifaa vya kufundishia ni vyombo muhimu katika kufunza.

Tulipowauliza walimu kuhusu vifaa vya kufundishia, kwanza kuhusiana na vitabu, walimu 12(60%) kati ya walimu 20 tuliowahoji walikuwa na malalamiko kadha. Wengi wa wale waliolalamika walisema kwamba walimu wakuu wa shule hawapendelei kununua vitabu vya Kiswahili. 6 kati ya hawa walisema kwamba wanafunzi hawana vitabu hivyo, huwalazimu walimu hawa kuandika fungu la kazi ubaoni. Wakati wa somo la fasihi huwalazimu kuwasomea wanafunzi kitabu. Hili ni jambo la kusikitisha sana. Lakini jambo hili, walieleza walimu, lilitokana na jinsi Kiswahili kilivyokuwa kikididimizwa na kudunishwa hapa nchini Kenya tangu enzi ya ukoloni.

Katika sura ya pili tuliona kwamba huku kudidimizwa na kudunishwa kwa lugha ya Kiswahili mazao yake ni zile sera za lugha tulizorithi kutoka kwa wakoloni. Na hata baada ya uhuru hizo kasumba za kikoloni hazikudidimia bali ziliendelea 'kupaliliwa na kuota mizizi'. walimu wengi walitumaini kwamba mabadiliko yaliyoletwa na mfumo wa elimu wa 8-4-4 huenda ukabadilisha mawazo ya wakuu wa shule na kuwafanya kukipa umuhimu Kiswahili kama masomo mengine.

Kwa upande wa vifaa vya kufundishia walimu wote walidai kwamba hili ni jukumu la Taasisi ya elimu ya Kenya (Kenya Institute of Education). Hata hivyo walidai kwamba taasisi hiyo haitekelezi jukumu lake kama inavyostahili, kwa sababu hiyo inawalazimu walimu kujitengenezea vifaa vyao wenyewe ili kurahisisha kazi ya ufundishaji. Lakini kati ya hao, walimu 20 waliyohojiwa,walimu 17 (85%) walikiri kwamba huwa hawatumii vifaa vya kufundishia. Kwa mfano wengi walidai kwamba hawatumii kanda ya kunasia sauti au michoro.

Tunaonelea kwamba, kwayo vifaa vya kufundishia ni ala muhimu sana katika kufundishia. Katika sura ya pili, tulitoa kauli kwamba ili mradi wo wote uweze kufanikiwa vifaa vya kufundishia ni vyombo muhimu sana. Hivyo, vifaa kama vitabu na vinginevyo ambavyo ni muhimu katika somo la Kiswahili yapaswa vinunuliwe na wale ambao wanahusika.

Ukosefu wa vifaa vya kufundishia una madhara yake. Ukosefu wa vitabu kwa mfano waweza kufanya mwalimu afe moyo, pili, waweza kuwafanya wanafunzi kukosa hamasa ya somo. Jambo kama hili laweza kuathiri matokeo ya mwanafunzi katika somo hili. Kwa mfano katika shule tulizotembelea, mbili kati yake tulionelea kwamba ingekuwa na matokeo ya kuridhisha iwapo ingekuwa na vitabu vya kutosha. Hizi ni shule ambazo walimu walilalamika kwamba hawana vitabu. Walimu walinieleza kwa kuridhika kwamba katika matokeo yao ya mwaka wa jana (1991) waliwahi kupata A moja katika kila shule, B zaidi ya ishirini,

C kama 25 na D chache lakini hawakupata E hata moja.

Hili ni jambo la kutia moyo. Ni wazi kwamba iwapo wanafunzi hawa wangekuwa na vitabu labda matokeo yao yangekuwa bora zaidi. Hivyo tunaonelea kwamba ingekuwa bora kama jambo hili lingerekebishwa na wale ambao wanahusika.

### 3.2.3. SILABASI

Tulipowahoji walimu kuhusu silabasi ya Kiswahili iliyotolewa kwa minajili ya mfumo wa 8-4-4, wengi walikuwa na sifa nyingi kuhusiana na silabasi hii. Hata hivyo, wengine walikuwa na wasiwasi wao kuhusu baadhi ya mambo yatakayofunzwa.

Tulipopitia madhumuni ya jumla kwa pamoja, kati ya walimu 20, walimu 16 (80%) walidai kwamba ni vigumu sana kulenga baadhi ya madhumuni.

Wengi walitoa mfano wa lengo la 'Kumwezesha mwanafunzi kuelewa na kuthamini fani mbali mbali na tamaduni'.

Walitoa kauli kwamba, hapa nchini hatuna utamaduni tunaoweza kudai kwamba ndio utamaduni wa Kenya. Kinachopatikana ni utamaduni kutoka jamii mbali mbali za wakenya. Hivyo hawakujua ni nini walichotakiwa kufunza ili kulenga shabaha hii.

Kuhusiana na yaliyomo, walimu 18 (90%) walionelea kwamba ingekuwa bora kama somo la Kiswahili lingeongezewa vipindi hasa katika kidato cha tatu na nne. cha

Sehemu ambazo walimu wanapaswa kutilia mkazo ni kusikiliza na kuongea, sarufi na msamiati pamoja na kusoma na kuandika.

Madhumuni ya mwanafunzi katika kusikiliza na kuongea ni kumwezesha mwanafunzi kuongea lugha kwa ufasaha. Katika sehemu hii walimu watakuwa na jukumu kubwa la kuwafunza ama kuwaongoza wanafunzi kujenga msamiati ufaao watakaoutumia katika maongezi yao. Wanafunzi nao wanajukumu la kujifunza msamiati wa aina mbali mbali watakaoweza kutumia katika siku za baadaye.

Lakini jambo linalowatatiza walimu ni kwamba sehemu hii inahitaji ujuzi mwingi wa Ki-Isimu. Kati ya walimu 20 tuliowahoji, 15 (75%) walisema kwamba hawajafanya Isimu. Walieleza wasiwasi wao katika kufundisha mambo kama vile matamshi, shada na tanakali za sauti. Kati ya walimu hao 15 ambao hawajafuzi, 10 walikiri kuwa na matatizo ya kufundisha sehemu hii kutokana na athari ya lugha ya kwanza.

Maoni yetu ni kwamba iwapo mwalimu ana matatizo haya atakuwa na tabia ya kukwepa kazi yo yote inayomlazimu aongelee kuhusu msamiati, matamshi au tanakali za sauti. Jambo hili linapotokea litaathiri sehemu hii.

Sehemu hii endapo itafunzwa ipasavyo itamwezesha mwanafunzi kukuza uwezo katika:-

i) Kubuni na kujieleza wazi kimantiki kwa kuzungumza na kuandika.

ii) Kusoma kwa ufasaha na ufahamu.

Hii ni baadhi ya madhumuni ya jumla yanayopaswa kutimizwa.

Fani nyingine ambayo imewekewa mkazo ni ya fasihi simulizi. Fani hii inamhitaji mwalimu kufundisha nyimbo, methali na vitendawili.

Walimu walidai kuwa haikufafanuliwa ni nyimbo za aina gani zinapaswa kufundishwa. Lengo maalum la kuanzisha somo la aina hii ni kuendeleza utamaduni wetu na kujenga umoja hapa nchini Kenya. Lakini kama tulivyokwisha kusema walimu wote tuliowahi kuongea nao walidai kwamba 'Hatuna utamaduni wa Kenya'.

Jambo linalowasumbua walimu ni kwamba endapo watafunza nyimbo, nyimbo hizo ni zipi? Ni zile za kikabila au ni zile za Kiswahili. Walimu wote 20 tuliowahoji walisema kwamba, endapo watafunza nyimbo za makabila labda watakuwa walienda kinyume cha kanuni ya serikali. Isitoshe walimu 17 (85%) walidai kwamba ni aina gani ya nyimbo za Kiswahili wanapaswa kufundisha. Walimu wote tuliowahi kuwahoji walisema kwamba ingefaa wafafanuliwe zaidi kuhusu jambo hili.

Fani nyingine ambayo inapaswa kufundishwa ni 'Historia ya Kiswahili'. Walimu 18 (90%) walionelea kwamba sehemu hii haipaswi kufundishwa katika shule za upili. Walitoa sababu kadha, kwanza walitoa kauli kwamba muda uliopewa somo la Kiswahili hautoshi.

Pamoja na hayo, waliona ya kwamba sehemu hii igefaa zaidi kufundishwa katika vyuo vya elimu ya juu. Kwa mfano, chuo kikuu.

Lakini sababu kuu waliotoa ni kwamba kutoka mfumo wa elimu wa 8-4-4 kuanzishwa swala la historia ya Kiswahili halijawahi kuulizwa kwenye mtihani. Hivyo walimu hawakuona umuhimu wa kufundisha sehemu hiyo.

Kutokana na yale tuliyopata kuhusiana na sehemu hii tuliona kuwa kuna hatari ya walimu wengine kutofundisha sehemu hii. Tungeshauri kwamba, sehemu hii ifundishwe uapo haitahiniwi. Tunaonelea kwamba kuna umuhimu wa kufundisha sehemu hii. Kwanza kutampa mwanafunzi msingi bora, pili mwanafunzi ataweza kumaizi kwa nini lugha ya Kiswahili haipewi hadhi sawa na kiingereza, mwisho kwa nini tuwe na lugha moja ya taifa.

Hivyo sehemu kama waswahili ni nani? uswahilini ni wapi, lahaja mbali mbali za Kiswahili pamoja na Kiswahili enzi za ukoloni na baada ya uhuru ni sehemu muhimu kufunzwa. Isitoshe, swala kwa nini tuwe na lugha mmoja ya taifa ni muhimu kufunzwa.

Linalopaswa kueleweka ni kwamba, jambo muhimu katika elimu, si kumwelimisha mwanafunzi yale atakayotahiniwa, bali ni kumwezesha mwanafunzi kuwa na ujuzi wa somo na zaidi ya hayo kumwelimisha yale yatakayomsaidia katika maisha ya baadaye.

Katika upande wa kusoma wanafunzi watakikana wajizoeze kusoma kwa ufasaha. Pia yatarajiwa kumwezesha mwanafunzi kuelewa umuhimu wa lugha; kufurahia aina mbali mbali za fasihi na kuwa na ilhamu ya kusoma kwa ziada kwa minajili ya kupanua ujuzi wake katika kusoma.

Katika hojaji iliyotayarishwa kwa ajili ya wanafunzi, kati ya wanafunzi 150, wanafunzi 122(81%) walikiri kwamba wanapenda kusoma vitabu vya Kiswahili. Tulipowahoji walimu kuhusiana na jambo hili wengi walikubali kwamba ikilinganishwa na wanafunzi wa hapo awali (yaani wa mfumo wa 7.6.3.) yaelekea kwamba kuna tofauti kubwa sana kati ya wanafunzi wa mifumo hii miwili. Walidai kwamba ilikuwa ni nadra sana kumwona mwanafunzi akisoma kitabu kilichoandikwa kwa Kiswahili. Lakini katika kipindi hiki utakuta wanafunzi wengi wakisoma.

Kuhusiana na kuunganishwa kwa 'Fasihi ya Kiswahili' na 'Lugha ya Kiswahili' kati ya wanafunzi 150, wanafunzi 64 (43%) walionelea kwamba si vizuri kufungamanisha 'lugha ya Kiswahili' na 'Fasihi ya Kiswahili. Sababu walizotoa ni kwamba ama fasihi ni somo ngumu hasa sehemu ya mashairi au waliona kwamba somo lenyewe linakuwa ni pana mno na halipewi vipindi vingi kama kiingereza.

Ni Wanafunzi 13 (8%) ambao walidai kwamba hawajui. Ni wanafunzi 77 (59%) waliona kwamba kuna umuhimu wa kufungamanisha masomo haya mawili.

Wengi walionekana kusema kwamba masomo yote mawili yanavutia hivyo hawaoni haja ya kutenganishwa.

Kati ya walimu 20 tuliowahoji, walimu 16 (18%) walisema kwamba masomo ya fasihi na Kiswahili hayapaswi kuunganishwa. Sababu walizotoa ni kwamba, muda uliotengewa somo hili hautoshi. Hapo zamani masomo haya mawili yalipewa jumla ya vipindi 7 kwa juma. Lakini baada ya kuunganishwa kwa masomo haya mawili, jumla ya vipindi viwili vilipungua. Vile vile walidai kwamba baadhi ya wanafunzi walikuwa wakifanya vizuri katika somo moja kuliko jingine. Hili liliwarudisha nyuma baadhi ya wanafunzi.

Wengine wao walikiri kwamba, walikuwa wamefuzu ama fasihi au lugha. Hivyo walikuwa wakikabiliwa na matatizo katika kufundisha sehemu ambayo hawajafuzu. Ni 20% ya walimu walishauri kwamba, 'lugha ya Kiswahili' humpa mwanafunzi msingi bora wa kujieleza katika fasihi. Kwa mfano, 'lugha' humsaidia katika zile sehemu za 'matamshi, tanakali za sauti na msamiati'.

Maoni yetu ni kwamba, wazo la kuunganisha masomo haya mawili halikuwa baya.

Lakini kama wengi wa walimu walivyosema kitendo cha kuunganisha masomo yote mawili kiliharakishwa mno. Ingelikuwa jambo la busara iwapo walimu wangeshauriwa kwanza. Pamoja na haya, yaonekana wazi kwamba kuna hatari ya kuwa baadhi ya walimu waweza kuwa wakifundisha sehemu moja huku wakisahau nyingine.

Walimu wote tuliowahoji walisema kwamba, silabasi iliyotayarishwa kwa minajili ya kufundisha Kiswahili katika shule za upili imepangika vyema. Vile vile, walisema kwamba kuna muumano kati ya yaliyomo na shabaha zilizowekwa kwenye silabasi.

Lililobaki ni namna ya kutafuta mbinu mwafaka ili kuwezesha mambo haya yaoane kama ilivyonuiwa.

## 3.2.4 HISIA ZA WANAFUNZI KUHUSU KISWAHILI

Kati ya wanafunzi 150, wanafunzi 118 (89%) walisema kwamba hufurahia somo la Kiswahili. Walitoa sababu kadha, wengi walisema kwamba ni lugha ya taifa, wengine wakasema kuwa ni lugha ya nchi yao, ambapo wengine walitoa madai kwamba Kiswahili hurahisisha mawasiliano miongoni mwa watu wa Kenya. Isitoshe ndiyo lugha ambayo kwayo inaweza kumaliza ukabila hapa nchini Kenya.

Wanafunzi 16 (11%) ambao walisema kwamba hawafurahii somo la Kiswahili walikuwa na haya ya kusema: somo la Kiswahili ni gumu kulielewa.

Yaelekea kwamba wanafunzi wameanza kubadilisha hisia zao kuhusu somo la Kiswahili. Idadi kubwa ya wanafunzi wanaionea fahari lugha ya Kiswahili. Sababu walizotoa zathibitisha kauli kwamba Kiswahili ndiyo lugha ambayo kwayo yaweza kumaliza ukabila hapa nchini Kenya. Hii ni kauli nzito.

Yaonekana pia kwamba, kwa kiasi fulani mwalimu ana doria ya kumfanya mwanafunzi ama kupenda somo au kutolipenda. Kuna baadhi ya wanafunzi waliotoa kauli kwamba, wao wanafurahia somo la Kiswahili kwa ajili ya walimu wao kuwashawishi. Maoni haya yanatilia mkazo swala ambalo wanafunzi walitakiwa kusema iwapo walimu wao waliwashawishi wafanye kazi yao ya Kiswahili kwa bidii. Kati ya wanafunzi 150, wanafunzi 130(87%) walikiri kwamba walishawishiwa.

Kati ya wanafunzi 150, wanafunzi 79 (52%) walikiri kwamba wanapenda Kiswahili hivi kwamba wao hujifunza wakati wanapopumzika. Vile vile kati ya wanafunzi 150, wanafunzi 122(81%) hupenda kusoma vitabu vya Kiswahili.

Yaelekea kwamba idadi ya wanafunzi wanaokipenda Kiswahili yaenda ikiongezeka hasa tukilinganisha na wanafunzi waliopitia mfumo wa hapo awali, yaani 7.6.3.

### 3.2.4.1. UMUHIMU WA KISWAHILI KWA WANAFUNZI

Vile vile wanafunzi waliulizwa iwapo masomo ya Kiswahili na kiingereza yana manufaa yo yote

kwao baada ya kumaliza shule. Wanafunzi 113(75%) kati ya 150 walisema 'kweli' au 'kweli kabisa' kuwa Kiswahili kina manufaa kwao. Wengi wao walisema kwamba kingewasaidia kazini katika kuwasiliana na watu ambao hawajui kiingereza. Maoni haya yalitiliwa nguvu na majibu ya swali la 19 ambapo 93% ya wanafunzi walikubali kwamba wangependa kupata kazi ambayo ingewabidi kutumia Kiswahili kila mara. Hivyo 70% walikiri kwamba wao hujaribu kufanya bidii ili kuongezea ujuzi wao katika Kiswahili. Sababu walizotoa ni kwamba ndiyo lugha ya taifa hivyo ni muhimu kuifahamu na wengine wakasema kwamba ndiyo lugha ambayo wanaweza kuwasiliana na kila mtu.

Katika kiingereza, wanafunzi 125 (83%) kati ya 150 walikubali kuwa kiingereza kina manufaa kwao. Walisema kwamba, kiingereza kingewasaidia katika kupata kazi, pili ndio lugha ambayo hutumika maofisini. Isitoshe, kuna ambao walisema kwamba kiingereza humpa mtu hadhi ya juu iwapo anakifahamu. Swala kuhusiana na kufanya bidii ili kuongezea ujuzi wao katika kiingereza 81% ya wanafunzi ilidai kwamba huwa wanafanya bidii.

Tukiangaza kwa macho makali, tutaona kwamba hisia za wanafunzi zaenda zikibadilika. Idadi ya wanafunzi ambao wanaona umuhimu wa lugha hii ya Kiswahili imeongezeka.

Tulipowahoji walimu walikubali kwamba hisia za wanafunzi kuhusu Kiswahili zaenda zikibadilika.

Kauli hii walitoa baada ya kuwalinganisha na wanafunzi waliopo sasa na wale wa hapo zamani. Walimu walisema kwamba, wanafunzi wa hapo zamani hawakuona manufaa yo yote katika kufanya somo la Kiswahili. Wengi walisikika wakiuliza "mwalimu, nikichagua kufanya Kiswahili hadi kiwango cha juu ninaweza kwenda katika chuo kikuu nikachukua kosi ya shahada ya juu ya Kiswahili?" Au wenye mabezo walisikika wakiuliza, 'mbona kwenye magazeti tunaona kazi zinatangazwa kila mara na kila wakati anatakiwa mtu aliyefanya vizuri katika hesabu, kiingereza na somo lingine? Mbona hawataki wale waliofanya vizuri katika somo la Kiswahili?"

Walimu walisema kuwa haya ni mazao ya sera za lugha tulizorithi kutoka kwa wakoloni. Kama tulivyoona katika sura ya pili Kiswahili kilionekana kama lugha ya kusema na 'maboi'. Kasumba hizi ziliendelea hata baada ya Kenya kujipatia uhuru.

Mfumo mpya wa elimu, ambapo Kiswahili kimefanywa somo la lazima, kwa kiasi tunaweza kusema kwamba umesaidia katika kuinua hadhi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Wanafunzi waliopitia katika mfumo huu wanajionea fahari kupata kazi ambayo itawabidi kutumia Kiswahili mara kwa mara.

Pia yawezekana kwamba kule kuandika fomu za kuulizia kazi kwa kiingereza upande moja na Kiswahili upande

mwingine **kunasaidia.** Pamoja na hayo kuna baadhi ya kozi ambazo zinahitaji mwanafunzi awe amefanya vizuri katika Kiswahili. Kwa mfano, kozi ya uandishi wa habari humlazimu mwanafunzi awe amefanya vizuri katika Kiswahili.

Maoni haya yanatiliwa nguvu na swala la 11 ambapo wanafunzi 135 (90%) waliona kuna umuhimu wa kuwepo kwa Kiswahili hata kama kiingereza kinaweza kutumika vizuri kwa kila kitu tukifanyacho. Hili ni jambo la kutia moyo. Yaelekea kwamba wanafunzi sasa wameanza kuona umuhimu wa kujifunza lugha hii.

Hivyo japo wanaona umuhimu wa kiingereza, lakini pia wanafahamu kuwa kuna manufaa ya kujifunza Kiswahili sio tu kwa manufaa ya mtu binafsi bali kwa taifa nzima kwa jumla.

## 3.2.4.2. USOMAJI WA MAGAZETI

Jumla ya wanafunzi 140 (93%) walidai kupenda kusoma magazeti na majarida yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili na kiingereza. Ni wanafunzi 10 (7%) tu ndio waliokiri kwamba hawasomi magazeti au majarida yaliyoandikwa kwa ama Kiswahili au kiingereza.

Jambo lililobainika kuhusu usomaji kwa jumla ni kwamba kati ya wanafunzi 140 ambao walidai kupenda kusoma makala fulani, 120 (80%).

Ni wanafunzi 20 (14%) ambao walisema kwamba wao hupenda kusoma magazeti katika lugha ya Kiswahili.

Jambo jingine ambalo lilijitokeza katika usomaji wa magazeti ni kwamba waliodai kupenda kusoma magazeti ya Kiswahili ni wanafunzi kutoka kidato cha nne tu.

Jedwali lifuatalo linawakilisha vizuri zaidi matokea ya majibu kuhusu usomaji wa magazeti

| GAZETI | | IDADI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Nation/Standard/Kenya Times | Kiingereza | 120 | 79% |
| Taifa Leo/Kenya Leo | Kiswahili | 20 | 14% |
| Aidha Kiingereza au Kiswahili | - | | |
| Hawasomi | - | 10 | 7% |
| Jumla | | 150 | 100% |

JADWALI LA 2

Wanafunzi wengi waliodai kutosoma magazeti katika lugha ya Kiswahili walipeana sababu kwamba katika shule wanakosoma, magazeti ya Kiswahili hayanunuliwi. Kwa wale wanaokwenda nyumbani walikuwa na dai hilo hilo kwamba nyumbani kwao magazeti ya Kiswahili hayanunuliwi.

Katika kundi hili la wanafunzi, maoni yetu ni kwamba labda wangeyapata magazeti haya wangeyasoma.

Kuna baadhi ya wanafuzi waliodai kwamba kusoma magazeti katika lugha ya Kiswahili huonekana kama mtu hajaelimika hivyo husushwa hadhi katika jamii. Kuligana na maoni haya, kundi hili la wanafunzi husoma magazeti ya kiingereza sio kwa sababu hawawezi kuelewa Kiswahili lakini ni kutaka kujinasibisha na tabaka la juu.

Maoni yetu ni kwamba sababu muhimu zaidi ya watu kusoma magazeti ya kiingereza ni huko kutaka kujitwika hadhi kuliko sababu yo yote nyingine. Ingawa walitoa sababu kuhusu swala hili.

Wanafunzi wanaopenda kusoma magazeti ya Kiswahili walitoa hoja kwamba wao hupendezwa na vituko vya kicheshi vya 'Juha Kalulu'.

3.2.4.3. USIKIZAJI WA RADIO

Hali kadhalika utafiti wetu ulituelekeza kwenye usikizaji wa radio. Wanafunzi wote walikiri kwamba husikiza radio.

Jambo lililodhihirika ni kuwa, hamna tofauti kubwa kati ya matokeo ya usikizaji wa radio na usomaji wa magazeti . 74% ya wanafunzi walidai kwamba wanapenda kusikiliza radio katika idhaa ya kiingereza. 24% ya wanafunzi ndio iliyodai kwamba husikia radio katika idhaa ya Kiswahili. Ni 2% tu iliyodai kwamba hupenda kusikiza radio katika idhaa ya lugha ya kwanza.

Usikizaji wa radio waweza kuonyeshwa vizuri katika jedwali lifuatalo.

| USIKIZAJI WA RADIO KWA LUGHA YA | IDADI | ASILIMIA |
|---|---|---|
| Kiingereza | 105 | 70% |
| Kiswahili | 36 | 24% |
| Aidha Kiswahili au Kiingereza | 7 | 4% |
| Lugha ya kwanza | 3 | 2% |
| Jumla | 105 | 100% |

JEDWALI LA 3

Ingawa wanafunzi wengi walidai kusikiza vipindi katika idhaa ya kiingereza, lakini tukiangalia kwa makini zaidi yaonekana kwamba hawajali sana vipindi vya kitaalam. Vipindi walivyotaja ni vya kuburudisha kuliko vipindi vinavyohitaji usikizi na fikra nyingi kuvielewa.

Wanafunzi walidai kusikiza vipindi katika idhaa ya kiingereza, lakini tukiangalia kwa makini zaidi yaonekana kwamba hawajali sana vipindi vya kitaalam. Vipindi walivyotaja ni vya kuburudisha kuliko vipindi vinavyohitaji usikizi wa fikra nyingi kuvielewa.

Wanafunzi ambao walidai kusikiza idhaa ya Kiswahili walionekana kupendelea vipindi ambavyo ni vya kielimu. Weingi walitaja vipindi kama 'Sanaa ya Kiswahili' na 'Maswali kwa Wanafunzi'. Wengine walitaja vipindi vya michezo ya kuigiza.

Jambo linalodhihirika kuhusu vipindi hivi ni kwamba baadhi ni vipindi vya nyimbo na vinginevyo sio vipindi

vinavyohitaji unyeti au usikizi wa makini.

Maoni yetu ni kwamba hawa ni watu ambao wangali vijana hivyo hawavutiwi na vipindi vyenye unyeti.

Kuhusu lugha wanayopendelea kutumia wakiwa darasani wanafunzi 60 (40%) walisema kwamba wanapendelea kutumia lugha ya kiingereza. Idadi ya wanafunzi 50 (33.3%) walidai kutumia Kiswahili. Jumla ya wanafunzi 40 '26.7%) walidai kwamba wao wanapendelea kutumia Kiswahili au Kiingereza.

Matumizi ya lugha ndani ya darasa yanaweza kuwakilishwa na jedwali hili.

| MATUMIZI YA LUGHA NDANI YA DARASA | IDADI | ASIMILIA |
|---|---|---|
| Kiingereza | 60 | 40% |
| Kiswahili | 50 | 33.3% |
| Kiswahili na Kiingereza | 40 | 26.7% |
| Jumla | 150 | 100% |

JEDWALI LA 4

Kuhusu lugha wanayopendelea kutumia wakiwa nje ya darasa, wengi walidai kwamba ilitegemea muktadha wa maongezi. Hata hivyo jumla ya wanafunzi 20 (13%) walidai kwamba wanapendelea kutumia kiingereza. Ni wanafunzi 50 waliodai kutumia Kiswahili lakini 20 kati yao walikiri kwamba wanapendelea kutumia sheng. Vile vile kuna wanafunzi 10 ambao walidai kupendelea matumizi ya lugha ya kwanza wakiwa nje ya darasa. Wengi wa wanafunzi walidai kwamba wanapendelea kutumia kiingereza, Kiswahili au sheng. Hawa walikuwa 70 (47%) kati ya wanafunzi wote.

Matumizi ya lugha nje ya darasa yanaweza kuwakilishwa na jedwali lifuatalo.

| MATUMIZI YA LUGHA NJE YA DARASA | IDADI | ASIMILIA |
|---|---|---|
| Kiingereza | 20 | 13% |
| Sheng | 20 | 13% |
| Kiswahili | 30 | 20% |
| Kiswahili na kiingereza na sheng | 70 | 46.6% |
| Lugha ya mama | 10 | 6.6% |
| Jumla | 150 | 100% |

JEDWALI LA 5

Kuhusu lugha waitumiao wakiwa nyumbani, wengi walisema kwamba wanapozungumzia nyanya au babu mara nyingi hutumia lugha zao za kikabila. Ni wanafunzi 5 tu waliodai kuwaongelesha wakitumia lugha ya Kiswahili.

## 3.3 UCHANGANUZI WA DATA

Katika sehemu hii tutajaribu kutoa uchanganuzi wa data iliyotolewa katika sehemu iliyotangulia. Tunatarajia kwamba uchanganuzi huu utatwelekeza kwenye kiini cha kazi yetu.

Kutokana na data tuliyoichukua, kuna mambo kadha yanayobainika kuhusu Kiswahili katika shule za upili. Tutaonyesha mambo haya na kuyafafanua zaidi katika sehemu hii.

Kwanza, jambo muhimu lililodhihirika katika utafiti wetu ni kwamba asilimia kubwa ya walimu na wanafunzi walionekana kukubali

kwamba jumla ya vipindi vinavyotengewa somo la Kiswahili havitoshi. Wengi walionelea kwamba Kiswahili kinapaswa kuwa na idadi sawa ya vipindi na kiingereza. Walimu walilalamika kwamba kiingereza kingali kinapewa umuhimu kuliko Kiswahili kwa kutengewa vipindi vingi.

Pili, walimu walidai kwamba Kiswahili katika shule za upili hakina vifaa vya kutosha vya kufundishia. Katika shule za watu binafsi (Private Schools) na shule za Harambee ilibainika wazi kwamba hakuna vitabu vya kutosha kwa wanafunzi. Wengi wa walimu kutoka shule hizi walisema kwamba, huwa wana kitabu kimoja tu cha mwalimu. Dai lilitolewa kwamba wakuu wa shule hawapendelei kununua vitabu vya Kiswahili.

Kuhusina na vifaa vingine vya kufundishia walimu wote walisema kwamba ni jukumu la Taasisi ya elimu ya Kenya kuvitoa. Hata hivyo walidai kwamba Taasisi hii haitekelezi jukumu lake inavyostahili. Huwalazimu walimu hawa kutengeneza vifaa hivyo wao wenyewe. Walitumaini ya kwamba jambo hili lingerekebishwa. Walisema kwamba ukosefu wa vifaa vya kifundishia waweza kuathiri kazi yao.

Tatu, kati ya walimu tuliowahoji, wengi wao walidai kwamba silabasi iliyotolewa kwa ajili ya Kiswahili katika shule za upili ni pana mno. Hivyo wengi walipendekeza nyongeza ya vipindi ili waweze kufundisha yote yaliyomo. Hata hivyo walikuwa na sifa nyingi kuhusu silabasi hii.

Walimu hawa walisema kuwa kuna muoano mzuri kati ya shabaha na yaliyomo. Lakini walionyesha wasi wasi wao kuhusu sehemu nyingine za silabasi hii. Kwa mfano, wengi walidai kwamba hawajui ni nyimbo zipi wanapaswa kufundisha. Ni nyimbo za Kiswahili au za kikabila.

Sehemu nyingine walionelea kwamba inapaswa kutolewa katika silabasi ya shule za upili ni ile sehemu ya 'Historia ya Kiswahili'. Wengi walitoa rai kwamba ingefaa zaidi kama sehemu hii ingefundishwa katika viwango vya juu vya elimu kwa mfano, chuo kikuu.

Kuhusiana na kuunganishwa kwa somo la 'fasihi' ya kiswahili na 'lugha ya kiswahili', wengi wa walimu walionekana kutopendezwa na jambo hili, sababu walizotoa ni kwamba, vipindi vilivyotengewa somo hili havitoshi kufundishia sehemu hizi mbili. Hivyo walionekana wakipendekeza nyongeza ya vipindi hasa katika vidato vya 3 na 4.

Ilidhihirika pia kwamba baadhi ya walimu hawajiamini wanapofundisha ama 'fasihi' au 'lugha'. Walisema kwamba ama wamefuzu katika fasihi au lugha lakini si zote mbili. Tulionelea kwamba kuna hatari ya walimu kama hawa kutilia mkazo sehemu moja huku wakipuuza nyingine.

Ilibainika pia kwamba wanafunzi wanamwelekeo au hisia za kuridhisha kuhusu Kiswahili. Uamuzi huu ulifikiwa kwa kutazama data hiyo kwa makini. Idadi ya wanafunzi waliosema kwamba wanafurahia somo la Kiswahili ni ya kuridhisha. Vile vile wanafunzi hawa walitoa madai kwamba wangependelea kupata kazi ambayo ingewalazimu kutumia Kiswahili kila mara.

Isitoshe, wengi walisema kwamba wanapenda kusoma vitabu vya Kiswahili.

Kuhusu iwapo Kiswahili kina manufaa yo yote, wanafunzi wengi walidai kwamba Kiswahili kina manufaa kwao katika maisha ya baadaye. Kwa mfano, kitawasaidia kuwasiliana na watu kazini. Hii ni kinyume na hali ilivyokuwa hapo zamani. Wanafunzi wengi waliofuzu katika mfumo wa elimu wa 7.6.3. walifikiri kwamba ili kupata ufanisi maishani, ni kiingereza tu ambacho kilikuwa na uwezo huo wa kuwafikisha katika ufanisi huo.

Vile vile tulifikia uamuzi huu baada ya kuona zile hoja walizotoa wanafunzi kuhusu hakuna haja ya kuimarisha Kiswahili kwa sababu kiingereza kipo. Wengi wa wanafunzi hawakukubaliana na kauli hii, wengi waliona kuna umuhimu wa kukiimarisha Kiswahili hasa tuelewapo kwamba ndiyo lugha ya taifa.

Yaelekea kwamba wanafunzi wameanza kuionea fahari lugha ya Kiswahili. Kauli walizotoa kuhusu Kiswahili zatuelekeza kusema hivyo. Idadi kubwa ya wanafunzi ilionekana kupenda Kiswahili kwa sababu ndiyo lugha ya taifa au kwa sababu ndiyo lugha ambayo inaweza kumaliza ukabila hapa nchini Kenya. Pamoja na hayo, wengine waliona lugha ya Kiswahili ikirahisisha mawasiliano miongoni mwa watu wengi hapa Kenya.

Kuna mambo kadha yaliyobainika kwenye utafiti wetu:

1) Sera za lugha ya elimu hapa nchini Kenya imekuwa na athari kubwa kwa Kiswahili.Utawala wa nchi ndio huamua lugha itakayotumika katika shughuli zote za kielimu. Utawala wetu nchini Kenya ulipendelea matumizi ya kiingereza katika shule ndiposa kiingereza kikawa ni lugha ya kutukuzwa. Hivyo ikawa ni muhimu kufuzu katika somo la kiingereza ili nafasi ya kupata kazi au nafasi katika elimu ya juu ipanuke. Kiswahili kiliwekwa kwenye matawi ya chini. Bila shaka tukio hili liliathiri somo la Kiswahili katika shule za upili.

2) Aina ya shule vile vile ina athari zake. Hadi wakati wa kujinyakulia uhuru nchini Kenya mwaka wa 1963 shule zilikuwa ni za kitabaka. Shule za tabaka la juu ambalo lilikuwa zaidi ni wazungu na wahindi pamoja na wafrika wachache walikuwa na sera ya lugha ya elimu ilizingatia maslahi yao. Lugha iliyotukuzwa mno ni kiingereza na kwa hivyo wanafunzi wa shule hizo walihimizwa 'wakiabudu' kiingereza na kukidharau Kiswahili. Hii ina maana kuwa wao hawakukutana na somo hili kabisa katika mkururo wao wa elimu. Jambo hili liliendelea hadi miaka ya themanini Kiswahili kilipoanza kupanda ngazi kama somo muhimu na la lazima katika baadhi ya viwango fulani vya elimu.

Kwa kuhitimisha uchanganuzi huu; tungependa kutahadharisha kwamba uchanganuzi huu ulitokana na data tuliyoikusanya na kuifafanua awali. Msingi wake ni matokeo ya majibu katika hojaji yetu.

Pili, wazo letu ni kwamba mfumo wa elimu wa 8-4-4 ambapo sasa Kiswahili ni somo la lazima kwa kiasi umesaidia katika kubadilisha hisia za wanafunzi kuhusu somo la Kiswahili. Jambo hili linaweza kusaidia katika kukikuza na kukiimarisha Kiswahili hapa nchini Kenya.

Tunatumaini kwamba yale yaliyobainika kuhusu Kiswahili katika shule za upili yanalingana na sehemu zingine hapa nchini Kenya. Ama kwa hakika kuna sehemu zingine hapa nchini ambazo haziwezi kulinganishwa na jiji la Nairobi kwa ambavyo mambo yatendwavyo na vifaa vilivyoko katika jiji hili.

## 3.4. MATATIZO YANAYOKABILI KISWAHILI NA MATATUZI YAKE

Kunayo matatizo kadha yanayokumba somo la Kiswahili chini ya mfumo wa 8-4-4. Kazi yetu yahusu kuchunguza Kiswahili katika shule za upili, hasa tutazingatia mambo yanayoweza kukwamiza uimarikaji wa Kiswahili katika shule za upili. Kwa hivyo katika sehemu hii tutachunguza matatizo yanayowakabili walimu na wanafunzi katika shule za upili.

### 3.4.1 TATIZO LA VITABU

Tatizo kubwa ambalo limewakumba walimu wa Kiswahili kwa muda

mrefu ni upungufu wa vitabu vya kutosha kufundishia somo hili. Jambo la kwanza linalosababisha upungufu wa vitabu vya Kiswahili ni ule umuhimu wa Kiswahili na mahala pake wakati wa kutumikia umma.

wachapishaji wengi wa vitabu hapa nchini walilielewa hili toka mwanzo na ndipo ikawa kwamba wachapishaji wengi hawako tayari kuchapisha vitabu vya Kiswahili bila kujua kama kitanunuliwa au la .

Tatizo jingine linalosababisha uhaba wa vitabu vya Kiswahili katika shule ni kule kutopewa umuhimu na wakuu wa shule. Walimu wengi hulalamika kwamba wakimpelekea mkuu wa shule orodha ya vitabu vya Kiswahili vinavyotakikana; mara nyingi hujibiwa kwamba 'shule haina pesa ya kununua vitabu'. Jambo linaloudhi ni kwamba, masomo mengine kama kiingereza hununuliwa vitabu bila ya pingamizi lo lote.

Jambo la kuzingatia ni kwamba masomo yote ni sawa. Iwe ni somo la Hesabu, kiingereza au Kiswahili. Hivyo swala la kubagua ni masomo yepi yanapaswa kununuliwa vitabu, halipaswi kuwepo. Hasa kwa wakati huu ambapo Kiswahili kimewekwa katika kundi la masomo ya lazima.

### 3.4.2 TATIZO LA WALIMU

Shida nyingine inayowakabili walimu wa somo hili ni upungufu wa walimu waliofuzu.

Isitoshe tunaona kuwa hata walimu wachache tulionao, wengi wao walijifunza Kiswahili kupitia lugha ya kiingereza. Hili ni tatizo kubwa.

Kwa sababu ya ukosefu wa walimu waliofuzu katika somo hili, walimu wa masomo mengine kama sayansi, hesabu na jiografia huidhinishwa kufundisha Kiswahili hata kama hawana ujuzi wo wote. Hii ni kwa sababu watu wengi wana imani kwamba mtu ye yote anaweza kuongea Kiswahili. Katika kutafiti kwetu, tuligundua walimu wawili wa somo la kiingereza waliokuwa wakifunza Kiswahili wakati kukiwa na upungufu wa walimu wa Kiswahili. Mantiki itumikayo ni kwamba Kiswahili ni somo jepesi.

Wakati umewadia wa kuchunguza upya na kurekebisha mawazo haya. Ingefaa wizara ya elimu ifikiriye upya kuwaajiri walimu waliofuzu.

### 3.4.3 <u>TATIZO LA KUUNGANISHA SOMO LA 'FASIHI YA KISWAHILI' NA 'LUGHA YAKISWAHILI'</u>.

Tatizo jingine latokana na kuunganishwa kwa somo la 'fasihi' na somo la 'lugha ya Kiswhili'. Kama tulivyotangulia kusema ni jambo la busara kuyaunganisha masomo haya. Lakini kuna mushkil ndani yake. Walimu wengi hawawezi kuyafundisha masomo haya kimseto.

Hapo juu nimegusia juu ya swala la uhaba wa walimu wa somo hili.

Hivyo basi inajiri kwamba katika shule ambayo ina mwalimu mmoja wa Kiswahili na mwegemeo wake upo upande wa fasihi, ataona shida kubwa itakapokuja kufundisha lugha. Mwalimu anayependa sana 'lugha' ataona vigumu kufundisha 'fasihi' hasa ikizingatiwa kwamba hajui mbinu za kufundishia 'fasihi'.

Hivyo basi kuunganishwa kwa masomo haya mawili kutawatatiza baadhi ya walimu .

### 3.4.4. WAZAZI KUFIKIRIA KUWA KISWAHILI HAKIFAI

Tatizo hili ni mbaya sana. Limerithiwa na wale walioathiriwa sana na kulevyo na kasumba za kigeni. Siku moja mzazi aliniuliza kozi ninayofanya katika chuo kikuu. Nilipomweleza kuwa ninafanya Kiswahili alionyesha nyuso ya mshangao. Kisha akaniuliza 'Kiswahili kitakusaidia vipi katika maisha ya baadaye?' Ndiposa, aliponieleza alikuwa na kijana katika shule ya upili aliyekuwa akifanya vizuri sana katika somo la Kiswahili. Ajabu ni kwamba, alikuwa akimkemea kila wakati na kumuuliza kwa nini asifanye vizuri katika kiingereza, kwani kwake yeye haoni umuhimu wowote wa somo hili la Kiswahili.

Kwa wazazi kama hawa wanapaswa kushauriwa kwamba kuna umuhimu wao kama wazazi kusaidiana na walimu hasa katika kumjengea mwanafunzi msingi imara katika maisha yake ya baadaye. Hili linawezekana ikiwa mzazi anashikilia ya kwamba masomo yote yatolewayo shuleni mtoto wake ayafanye na lsitoshe, ayafanye vizuri.

## SURA YA NNE

## HITIMISHO

4.0 Katika sura hii tutatoa maoni na mapendekezo kuhusu matokeo ya utafiti wetu. Tungetaka kutanabahisha kwamba maoni hayà yanatokana na data tuliyoikusanya iliyoko katika sura ya tatu.

### 4.1 YALIYOBAINIKA KUTOKANA NA DATA

Katika tasnifu hii, tulikataa kujifunga na nadharia moja. Badala yake tulichukua dhana za ujuzi (competence) na uwezo (performance) wa lugha Chomsky (1965) na uwezo katika mawasiliano (Communicative Competence) ya Hymes (1974).

Ilibainika kuwa sifa za mtu kuijua lugha hutegemea ule uwezo wake wa kuitumia na kuisarifu. Lakini jambo hili, linategemea mambo mengi. Kwa mfano, mazingira, hisia na mtazamo wa watu kuhusu lugha hiyo.

Katika eneo la utafiti wetu tumefaulu kuonyesha kwamba kuna masiala ambayo yanaweza kuwa vizuizi katika somo la Kiswahili.

Imedhihirika wazi kwamba muda uliotengewa somo la Kiswahili hautoshi. Walimu pamoja na wanafunzi walionelea kwamba ingekuwa ni jambo la busara kama wakati huo ungeongezwa. Tukilinganisha muda unaopewa kiingereza na Kiswahili yaonekana sio sawa. Yaelekea kwamba kiingereza kinapewa umuhimu kuliko

Kiswahili. Kutokupewa muda wa kutosha kwa somo hili kwamaanisha kwamba inakuwa vigumu sana kukamilisha silabasi kwa kipindi cha miaka minne. Hivyo walimu wengi walisema kwamba silabasi yenyewe ni pana mno. Kuna sehemu ambazo, walimu hawa waliona kuwa zingefaa kufundishwa kwa ukamilifu katika vyuo vikuu. Kwa mfano, ile sehemu ya Historia ya Kiswahili. Walimu walidai kwamba sehemu hii huwa haitahiniwi hivyo hawakuona umuhimu wa kuifundisha katika shule za upili.

Maoni yetu ni kwamba kuna umuhimu wa kufundisha sehemu hii. Tunaonelea kwamba, wanafunzi wataelewa na mambo kadha kuhusu Kiswahili kwa mfano, Asili ya lugha ya Kiswahili, maendeleo yake nchini Kenya na umuhimu wa lugha hii kama lugha ya taifa hapa nchini Kenya.

Jambo la kuridhisha ni kwamba kuna muoano/muumano mzuri kati ya yaliyomo na madhumuni yaliyowekwa katika silabasi. Yaani maudhui yaliyoandikwa katika silabasi yanaweza kusaidia katika kulenga madhumuni. Lililobaki ni jinsi ya kutafuta mbinu muafaka ili kuwezesha mambo haya yaoane kama ilivyonuiwa.

Vile vile utafiti wetu umeonyesha kwamba kuna upungufu wa vitabu vya somo la Kiswahili katika shule za upili. Ilidhihirika kwamba wakuu wa shule hawapendelei kununua vitabu vya Kiswahili bali huwaambia walimu wawahimize

wanafunzi kununua vitabu hivyo wenyewe. Wengi wa wakuu wa shule hulalamika kwamba hakuna fedha. Jambo la kushangaza ni kwamba wakuu hawa huonekana wakinunulia masomo mengine vitabu.

Uchunguzi wetu waonyesha, sababu ya wakuu hawa kutokuwa radhi kununua vitabu vya Kiswahili ni ule umuhimu unaopewa somo hili ikilinganishwa na masomo mengine kama vile ya sayansi au hesabu.

Ilithibitika pia kwamba, hakuna vifaa vya kutosha vya kufundishia. Kwa mfano, vifaa kama chati, radio na kanda za kunasia sauti. Walimu walidai kwamba ni jukumu la Taasisi ya elimu ya Kenya [(Kenya Institute of Education) (K.I.E.)] kupendekeza au kutoa vifaa hivi katika shule lakini Taasisi hii huwa haifanyi hivyo.

Kuhusu kuunganishwa kwa 'lugha ya kiswahili' na 'fasihi ya kiswahili' ilidhihirika kwamba walimu wengi wa somo hili wamemakinika katika sehemu moja kuliko nyingine. Hii ni kwa sababu walimu hawa walipitia mfumo wa hapo zamani ambapo mtu ama angefanya 'lugha ya Kiswahili' au 'fasihi ya Kiswahili' ilitegemea hiari ya mtu.
Katika swala hili la kuunganisha kwa masomo haya mawili, tulifikia uamuzi kwamba walimu hawa hawapendi masomo haya yafungamanishwe siyo kwa sababu hawaoni umuhimu wa kufanya hivyo bali wasi wasi wao mkubwa ulikuwa ni kufundisha sehemu

ambazo hawajafuzu.

Kutokana na utafiti wetu tulifikia uamuzi kwamba, kasumba tulizorithi kutoka kwa wakoloni hazijafutika kabisa miongoni mwa watu wengi. Wazo kwamba kuna lugha bora (kiingereza) kuliko nyingine (kiswahili) lingalipo. Ilidhihirika kwamba, kiingereza kina vipindi vingi (vinane) kuliko Kiswahili (vitano) katika juma moja.

Hata hivyo tukichunguza kwa macho makali itaonekana wazi kwamba kiingereza ndiyo lugha ya kisomo hapa nchini Kenya na isitoshe inaaminika kwamba ili kupata kazi yenye pato kubwa ni muhimu kwa mtu kufahamu kiingereza.

Katika sura ya kwanza, moja kati ya haipothesia zetu ilikuwa kwamba ukosefu wa vitabu, walimu na kasumba za kikoloni ni miongoni mwa matatizo yanayolikumba somo la kiswahili. Utafiti wetu uligundua kwamba katika baadhi ya shule hasa shule za watu binafsi, hamna vitabu vya kutosha vya kufundishia. Vile vile ilionekana kwamba kuna upungufu wa walimu waliohitimu kufundisha somo hili. Hivyo miongoni mwa shule tulizozitembelea tulielezwa kwamba walimu wa masomo mengine hulazimika kufundisha somo hili. Haya yote twaweza kusema kwamba kwa kiwango kikubwa yamesababishwa na zile sera tulizorithi kutoka kwa wakoloni. (Tazama sura ya pili). Utawala wa kikoloni ulikipinga kiswahili katika shule. Tuliona kwamba utawala huu ulihimiza matumizi ya lugha za kikabila katika viwango vya chini na kiingereza katika viwango vya juu.

Hata baada ya Kenya kuwa nchi huru, sera za lugha hazikubadilika sana. Kiingereza kiliendelea kutukuzwa huku Kiswahili kikifanyiwa juhudi chache sana.

Mpaka hapa, tumetimiza lengo letu ambalo lilikuwa kuonyesha masiala mbali mbali ambayo ni muhimu kutiliwa maanani ili kuimarisha somo la Kiswahili katika shule za upili.

Utafiti wetu umedhihirisha kuwa picha ya hapo awali imebadilika. Kiswahili si lugha ya kudharauliwa tena miongoni mwa wanafunzi. Hisia, mwelekeo na msimamo wa wanafunzi ni za kuridhisha.

Werdelin (1960) katika uchunguzi wake alioufanyia wanafunzi wa hesabu aliona kwamba matokeo ya mwanafunzi shuleni yanaweza kusababishwa na hisia alizonazo katika somo hilo na kwa upande ule mwingine matokeo hayo yanaweza kuathiri hisia za mtoto. Kwa mfano, mapendekezo na mashauri ya walimu, wazazi na mengineyo.

Katika utafiti wetu ilibainika wazi kwamba wanafunzi wana hisia za kuridhisha kuhusu somo la Kiswahili. Tunataraji kwamba matokeo ya wanafunzi yatakuwa bora tukiyalinganisha na matokeo ya wanafunzi waliopitia mfumo wa hapo zamani.

Tunaweza kusema kwamba mabadiliko haya hayakutokana na ombwe tupu.

Baadhi ya mambo yaliyowafanya wanafunzi kuwa na mwelekeo mzuri kwa Kiswahili labda ni pamoja na kukifanya Kiswahili kuwa somo la lazima katika mfumo wa elimu wa 8-4-4 kwa wakati huu somo la Kiswahili ni la lazima. Hivyo mwanafunzi anahitaji kujibidiisha katika somo hili kama yale mengine.

Pili, serikali ya Kenya imepiga hatua kwa kutoa sharti kwamba mpaka uwe umefuzu katika somo la Kiswahili ili uweze kujiunga na baadhi ya kozi (kwa mfano kozi ya uandishi wa habari). Awali kozi nyingi zilihitaji mtu awe amefuzu kiingereza, hesabu na somo jingine wala si Kiswahili.

## 4.2 MAONI NA MAPENDEKEZO

Kama tulivyodokeza katika sura ya kwanza na kuthibitisha katika sura ya tatu, kuna mambo ambayo yanapaswa kuzingatiwa ili Kiswahili kiweze kuimarika zaidi katika shule za upili. Vile vile kitendo hiki kitawasaidia wanafunzi kuimudu lugha ya Kiswahili. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tukisaidia jamii pana kwa ujumla.

Hatua ya kwanza na muhimu zaidi ni kuweko kwa sera imara ya lugha. Ni lazima mipango thabiti ya lugha ifanywe na kutekelezwa ipasavyo. Ni jambo la kushangaza kuwa nchini Kenya hakujakuwa na sera maalum hata ingawa lugha kama ya kiingereza, Kiswahili na nyingi za makabila zinaendelea kuchukua nafasi katika mfumo wetu wa elimu.

Ingawa upangaji wa sera ya lugha na utekelezaji wake zinagharimu pesa, ni swala linalotakiwa kuwekwa mbele miongoni mwa maswala muhimu ya taifa. Wataalam wa lugha - upangaji wake na sera yake wanatambua hatua mbili za kutimiza wajibu huo (mbaabu 1978). Kuna upangaji wa lugha kwa ndani. Hii ina maana ya kuistawisha lugha hiyo kwa njia kadha, kama vile uundaji wa makamusi na usanifishaji wa istilahi mbali mbali. Jukumu hili ni la wataalam wa lugha hiyo na lsmu. Hatua ya pili ni ya upangaji wa lugha kwa nje. Kiini chake hasa ni kuiangalia lugha hiyo katika muktadha wa mahitaji ya nchi kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Ni vizuri sera hiyo ipangwe kwa njia ambayo itasadia kutekeleza malengo na dhamira za kitaifa. Hatua hizi mbili ni muhimu kuzingatiwa kwa udhati. Tunapendekeza kuwa serikali ikubali kugharamia mpango wo wote wenye lengo la kustawisha lugha hasa ya Kiswahili. Tunahitaji angalau kamusi zinazofaa kwa wanafunzi wa shule za upili.

Tunahimiza pia ukaguzi na usimamizi wa ufundishaji wa Kiswahili uimarishwe. Hata hivyo tungependekeza kwamba ukaguzi huo uwe wenye kuwaonyesha walimu njia mbali mbali za kufundisha kiswahili badala ya kuwa ni kuwakemea na kuwatolea vitisho walimu. Wakaguzi wenyewe tungependekeza wawe ni watu wenye ujuzi na waliofuzu katika kazi yao.

Vile vile tungependekeza walimu wahudhurie kozi au semina fupi fupi ili waweze kufahamishwa mabadiliko yanayotokea

mara kwa mara katika somo hili.

Njia nyingine tunayoipendekeza katika juhudi za kukiimarisha Kiswahili ni uandishi wa vitabu vya kiswahili. Tunawahimiza wale wenye ujuzi wa kuandika waandike vitabu ili kupunguza ukosefu wa vitabu katika shule. Pia tungewashauri waandike vitabu na makala yanayohusiana na maisha yetu kwa lugha nyepesi ya Kiswahili.

Ili kuhakikisha kwamba utaratibu wa masomo watekelezwa bila shida, Mungania (1986) anatoa kanuni ambazo ni muhimu kufuatwa.

1. Kukusanya habari kuhusu mahitaji ya elimu. Jambo hili lahitaji utafiti wa kutosha ufanywe ili kuweza kutambua mahitaji ya jamii. Hakuna utafiti wa aina hii uliofanywa kabla ya kuanzishwa kwa mfumo wa elimu wa 8-4-4. Serikali ya Kenya ilihisi tu kwamba aina ya elimu iliyokuwa ikitolewa katika mfumo wa hapo zamani haikukidhi matakwa ya jamii. Hivyo wakaonelea wabadilishe.

2. Kuanzishwa kwa miradi ya kubadilisha utaratibu wa masomo. Jambo hili laweza kutekelezwa na kamati mbali mbali zilizochaguliwa.

3. Mipango halisi ifanywe kuhusu utaratibu wa masomo. Hili linahusu kuweko kwa madhumuni fulani, kuchagua mambo muhimu yatakayofunzwa.

4. Kustawisha na kukuza vifaa vya kutumiwa kufundishia kama vitabu, michoro, chati na kadhalika. Kwa hakika baadhi ya matatizo yanayokikumba Kiswahili hayangekuwepo kama jambo hili lingetiliwa maanani toka mwanzo.

5. Kuwaelimisha watu watakaohusika na utekelezaji wa mradi huo. Kwa mfano, kuwapeleka walimu semina fupi fupi ili wapate maarifa ya kutosha kuweza kukabiliana nao. Mfumo huu ulipoanzishwa walimu hawakujua waanze wapi, wafundishe nini na waache nini. Walijikuta wametwishwa mzigo wa kufundisha bila ya mwelekeo wo wote.

6. Kuujaribu mfumo huo kwa kuzichagua shule chache ili utaratibu huo uendeshwe huko kwa muda fulani ili kuonekana kama mfumo huo utafaulu. Kuwaarifu wananchi kuchagua vifaa vifaavyo na kuufanyia marekebisho pale inapohitajika. Hakuna jambo kama hili lililofanywa wakati wa kwanzishwa kwa mfumo wa 8-4-4, kamati ya Mackay ilipendekeza mabadiliko ya mfumo wa elimu mwaka wa 1981 na hapo mnamo mwaka wa 1982 mfumo wenyewe ukaanza kutekelezwa.

7. Kuna kule kutekelezwa kwa mfumo na hapo baadaye ni muhimu kuwe na ufuatilizi ili kuhakikisha mfumo huo wafaulu, pengine kwa kuwafanyiza wanafunzi mtihani.

Tunapoangalia kwa makini, tunaona kwamba hakuna utaratibu wo wote uliofuatwa ili kutekeleza mfumo wa 8-4-4.

Nia ya kuanzisha mfumo huu haikuwa mbaya lakini utaratibu uliofuatwa ndio uliokuwa mbaya. Tungeshauri wanaohusika kufuata utaratibu maalum katika utekelezaji wo wote wa mfumo wa elimu. Jambo kama hili laweza kusaidia katika kuepuka baadhi ya matatizo yanayoukumba mfumo mzima. Iwapo utaratibu kama huu ungefuatwa baadhi ya matatizo yanayokikabili Kiswahili katika shule za upili chini ya mfumo wa 8-4-4 hayangekuwepo.

Tunataraji kwamba utafiti wetu umetoa mwangaza kuhusu Kiswahili katika shule za upili. Katika jiji la Nairobi. Hali hii ni kielelezo cha hali ilivyo katika miji mingine yenye sifa karibu sawa na jiji hili. Hata hivyo tunaelewa kwamba kuna sehemu ambazo haziwezi kulinganishwa na jiji la Nairobi. Vile vile kazi yetu itawaongoza wengine ambao wangeamua kuendeleza utafiti huu katika sehemu nyingine za nchi na kufanya kazi ya kiulinganishi au kushughulikia vipengele vingine; kwa mfano, ufundishaji wa kiswahili katika shule za upili.

## 4.3 MATATIZO YA UTAFITI

Kuna matatizo kadha yaliyotukabili katika kufanya utafiti wetu, kwanza si wahojiwa wote waliokuwa tayari kusaidia kujibu maswali. Wengine hawakutaka kujibu maswali haya kwa sababu walihisi kuwa wakati wao wa kufundisha ulikuwa ukitumiwa.

Pili, hatukupata hojaji kwa wakati ufaao. Baadhi ya shule tulizotembelea ili kuchukua hojaji, tulikuta ya kwamba hata hojaji zenyewe hazijapewa wanafunzi. Hili liliturudisha nyuma.

Tatizo lingine lilitotukabili ni ukosefu wa fedha. Kazi hii yetu haikugharamiwa na chuo wala shirika lo lote lile kutoka nje. Hivyo niliwajibika kufanya kazi hii peke yangu. Kwa mfano, kupeleka na kuzichukua hojaji katika shule mbali mbali. Jambo hili pia liliturudisha nyuma.

MAREJEO


1. Abudulaziz, M.H.(1986): *Makala ya semina: Development and Technical Terminology with Special Reference to African Langauages.*

2. Allport, G.W. (1935) : *Attitudes: A handbook of social psychology*, (Ed Murchison) worcester.

3. Bhaiji, A.F. (1976) : "The Medium of Instruction in our secondary Schools" In papers In Education and Development N° 3 University of Dar-es-Salaam.

4. Bogonko, S.N. (1986) : English Language and Education in East Africa katika *Conference on English in East Africa*. The British Council, Nairobi.

5. Chiraghdin, S, et al (1977) : *Historia ya Kiswahili*, Nairobi, Oxford University Press.

6. Chomsky, N. (1965) : *Aspects of the theory of syntax*, Cambridge, Mass. M.T.T. Press.

7. Claessen, T. (1986) : *English Across the Curriculum* katika Conference on English in East Africa.

The British Council, Nairobi.

8. Durojaiye, M.O. (1976): *A New Introduction of Educational psychology*, Evans, London.

9. Fishman, J.A. (1972) : The Sociology of Language: Massachusetts, Newsbury House Publishers.

10. Freire, P.F. (1980) : Pedagogy of the Oppressed Middlesex, pergrim.

11. Gachathi, (chairman) (1976): : Report of the National Commission on Educational Objectives and policies Nairobi, Government Printers Kenya.

12. Gumperz, J.J. (1971) : Language in social Groups; Carlifornia, Standford University Press.

13. Halliday, M.A.K. (1976) : Systems and Functions in Language London, Oxford University Press.

14. Harries, L. (1976) : The Nationalization of Swahili in Kenya. Department of African Languages and Literature, University of Wisconsin, Madison katika language in society vol.5.

15. Hymes, D. (1974) : Foundations In Socialingustics An Ethnographic Approach, Philadelphia; University of Pennyslavian Press.

16. Ikumi, M.E. (1985) : Vifaa Vya Kufundishia na Kusoma katika shule za Msingi, Iveti Division. Unpublished P.G.D.E. Dissertation.

17. Jordan, D. (1941) : The Attitude of Central School Pupils to certain School Subjects and the Correlation between Attitude and Attainment, BJEP, Vol. xi, part 1.

18. Kenya Education Commission Report (Ominde), Part one, 1964.

19. Mackay, C.B. (Chairman) 1982: Second University In Kenya: Report of the Presidential Working Party. Nairobi, Government of Kenya.

20. Magawi, N.B. (1978) : Shida zinazokabili ufunzaji wa Kiswahili katika LUGHA: A journal for language Teachers in Kenya, Vol. 5, Nº 3.

21. Maganga, C. (1978) : Ufundishaji wa Kiswahili katika shule za Msingi, Sekondari, chuo kikuu Na vyuo vya walimu katika LUGHA, A journal for language Teachers in Kenya Vol.5 Nº 3.

22. Mazrui, Al - Amin, M. (1981) : Acceptability in a Planned Standard: The case of swahili in Kenya. Ph. D. Dissertation Standford University, U.S.A.

23. Mbaabu, I. (1978) : Language planning in Kenya: Some practical consideration, katika LUGHA, A journal for language Teachers in Kenya, Vol. 5, Nº 3.

24. Melaughlin, B.(1987) : Theories of second - language learning Edward Aknold (Publishers) Ltd. London.

25. Ministry of Education, Science and Technology (1984) : 8-4-4 System of Education Nairobi G.P.K. (1/12/84).

26. Ministry of Education, Science and Technology (1985) : Secondary Education Kiswahili Syllabus for K.C.S.E. Nairobi, K.I.E.

27. Mkangi, K.G.C. (1985) : The Political Economy of Kiswahili: A Kenya - Tanzania Comparison in J. Maw and D. Parkin (Eds) Swahili language and society Afro-pub, Wein.

28. Muganga, A. (1977) : Attitude and Motivations of Tanzania pupil learning French in Secondary School, M.A. Dissertation, University of France, Comte.

29. Mukhabi - Lutta, M.C. (1986) :
Lutta-Mukhebi, M.C,
The competencies of English language Teachers in secondary school in Kenya katika conference in English In East Africa. The British Council, Nairobi.

30. Mungania, B.G. (1986) ; Ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili chini ya mfumo wa 8-4-4 (KIDATO CHA KWANZA). Unpublished P.G.D. Dissertation. Kenyatta University.

31. Mutahi, K. (1978) : The Kiswahili syllabuses in Kenya Institution, katika LUGHA, a journal for language Teachers in Kenya, Vol.5, Nº 3. Publishers, wapi?

32. Muthiani, J. (1986) : History of language policy in Kenya katika Conference on English In E. Africa. The British Council., wapi?

33. Nabakwe, N.T. (1985) : Vitabu vya kufundishia lugha ya Kiswahili kidato cha kwanza, unpublished P.G.D.E. Dissertation., wher

34. Ngina, I.M. (1990) : Mtindo katika Matumizi ya lugha ya Kiswahili - Utafiti katika mtaa wa Pioneer Mjini Naïrobi. Unpublished. M.A. Dissertation. University of Nairob

35. Njogu, S.K. (1988) : Hisia za watu juu ya Kiswahili na hadhi wanayopatia lugha hii - utafiti katika kata ya magutu. M.A. Dissertatic University of Nairobi. (Unpulished)

36. Oliver, R. (1952) : The Missionary Factor in East Africa, Longman, London.

37. Richard, J.C. et al (1986) : Approaches and Methods In Language Teaching A description and Analysis, press syndicate of the University of

38. Syambo, K. (1978) : Ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za sekondari nchini Kenya, in LUGHA: a journal of Language Teachers in Kenya, Vol. 5, № 3.

39. Tippett, L.H.C. (1972) : Random Sampling Number (University College London), Department of Applied Statistics, Tracts for computers, № 15. Cambridge University Press London.

40. Wanyoike, E.N. (1978) : Vikwazo katika mafunzo ya Kiswahili Kenya, in LUHGA, a journal of Language Teachers in Kenya, Vol. 5 № 3.

41. Werdelin, I. (1960) : A Study of Factors Underlying Attitudes Towards and Interest in Mathematics and Schoolwork, Lund.

42. Whiteley, E.H. (1957) : Language and Politics in Kenya, Tanganyika Notes and Records, № 47/48.

43. ___________, (1968) : Language use and social change. Oxford University Press, London.

44. ___________, (1974) : Language in Kenya, Oxford University Press, Nairobi.

KIONGEZO (Appendix)

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

Idara ya Ismu na Lugha za Kiafrika

Machi 1992

Tungetaka kuomba msaada wako katika kujibu maswali yalioko katika Fomu hii. Majibu yako yatatusaidia kukamilisha utafiti tunaoufanya kuhusu: Kiswahili katika shule za upili:- (Utafiti katika jiji la Nairobi)

JINA____________________________

UMRI____________________________

SHULE___________________________

KIDATO__________________________

Katika maswali yanayofauta maagizo yametolewa. Penye chaguo la majibu weka alama (✓) kando ya lile ama yale yaliyomuafaka.

1. Unapendelea kutumia lugha gani ukiwa

   a) Darasani

   b) Nje ya Darasa

   c) Nyumbani

2. Unafurahia somo la Kiswahili?

   a) Ndiyo

   b) Hapana

a) Kama 'Ndiyo' kwa nini?

b) Kama 'Hapana' kwa nini?

3. Nafikiri ingefaa sana Kiswahili na Kiingereza kupewa idadi sawa ya vipindi katika shule.

a) Kweli kabisa

b) Kweli

c) Si kweli

d) Si kweli kabisa

e) Sijui

4. Nafikiri kuwa Kiswahili katika shule kinapewa muda mwingi ambao haufai.

a) Kweli kabisa

b) Kweli

c) Si kweli

d) Si kweli kabisa

e) Sijui

5. Si vizuri kufungamanisha somo la Kiswahili na Fasihi ya Kiswahili.

a) Ndiyo

b) Hapana

c) Sijui

6. Nakipenda Kiswahili sana hivi kwamba hujifunza wakati ninapopumzika.

a) Kweli kabisa

b) Kweli

c) Si kweli

d) Si kweli kabisa

e) Sijui

7. Napenda kusoma vitabu vya Kiswahili.

a) Kweli kabisa

b) Kweli

c) Si kweli

d) Si kweli kabisa

e) Sijui

8. Kila siku mimi hujaribu kufanya bidii kuongezea ujuzi wangu wa Kiingereza.

a) Kweli kabisa

b) Kweli

c) Si kweli

d) Si kweli kabisa

e) Sijui

9. Kiingereza kina manufaa yo yote kwako baada ya kumaliza shule?

a) Ndiyo

b) Hapana

9. a) Kama 'ndiyo' eleza.

10. Kila siku mimi hujaribu kufanya bidii kuongezea ujuzi wangu wa Kiswahili.

a) Kweli kabisa

b) Kweli

c) Si kweli

d) Si kweli kabisa

e) Sijui

11. Kiswahili kina manufaa yo yote kwako baada ya kumaliza shule?

a) Ndiyo

b) Hapana

11. a) Kama ndiyo eleza.

12. Je, ungekubali kuwa kwa sababu kuna kiingereza, hakuna haja ya kujifunza Kiswahili kwa sababu kiingereza kinaweza kutumiwa vizuri kwa kila kitu tukifanyacho.

a) Ndiyo

b) Hapana

13. Mwalimu wetu wa Kiswahili hutusawishi tufanye kazi yetu kwa bidii?

a) Ndiyo

b) Hapana

14. Ningependa kupata kazi ambayo ingenibidi nitumie Kiswahili kila mara.

a) Kweli kabisa

b) Kweli

c) Si kweli

d) Si kweli kabisa

e) Sijui

15. Je, wewe husoma magazeti au majarida mengine yo yote?

a) Ndiyo

b) Hapana

16. Yataje

a)

b)

c)

17. Ni idhaa gani inakupendeza zaidi katika radio ya sauti ya Kenya.

a) Taifa (Kiswahili)

b) Kiingereza

c) Lugha za kienyeji

18. Taja vipindi 5 ambavyo vinakuvutia zaidi katika sauti ya Kenya (K.B.C.)

a)

b)

c)

d)

e)

19. Ikiwa wafurahishwa na muziki, hupendelea nyimbo zilizoimbwa kwa lugha gani?

a) Kiswahili

b) Kiingereza

c) Lugha yangu ya mama

d) Nyingine

AINA YA MASWALI YALIYOULIZWA WALIMU

1. Kazi uifanyayo katika shule hii ni ipi?
2. Ujuzi wako katika kazi hii unatimia miaka mingapi?
3. Kuna walimu wangapi mnaosaidiana nao katika kufundisha Kiswahili hapa shuleni?
4. Jumla ya vipindi unavyofunza katika juma moja ni vingapi?
5. Je, unafikiri somo la Kiswahili linapewa muda wa kutosha? Toa sababu.
6. Je, unafikiri Kiswahili na Kiingereza kinapaswa kuwa na idadi sawa ya vipindi katika shule? fafanua.
7. Kuna haja ya kufungamanisha somo la 'Lugha ya Kiswahili' na 'fasihi ya Kiswahili'?
   b) Eleza
8. Je, silabasi iliyotayarishwa kwa minajili ya shule za upili yaweza kukamilika kwa muda wa miaka 4?
   b) Kuna muoano mzuri kati ya yaliyomo na madhumuni katika silabasi? Eleza.
9. Ni matatizo gani yanayokukabili katika kufundisha Kiswahili katika kidato cha kwanza, pili, tatu, na nne.
10. Ni vifaa gani unavyovitumia kufundishia kidato cha kwanza, pili, tatu na nne?
    b) Oredhesha vitabu vyote unavyovitumia katika kila kidato.
11. Je, ungependekeza mambo gani yafanywe ili kutatua matatizo yanayokukabili?
12. Una maoni yo yote ambayo ungependa kutoa kwa wananchi?